Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumatano Aprili 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580543
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Serikali** Zanzibar yazuia mabilioni ya kampuni upatu

UKURASA 5



**CCM** yang'ang'ania mgombea ubunge ACT- Wazalendo

UKURASA 5



Ukurasa 14
Siku 19 za Rais Samia zatengua msimamo wa Lipumba kususa

siasa
JUMATANO APRILI 7, 2021
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 12
MWANZO UHURU WA MSUMBIJI NCHINI

MZEE MASALAKULANGWA;
Nguzo ya CCM Kanda ya Ziwa amkubali Rais akimpa 'tano'
• Apima darubini yake, neema yaja

Na Anthony Gervas, MWANZA

SIKU zinazidi kuhesabika, Rais Samia Suluhu Hassan, yuko madarakani akiwa na mambo kadhaa aliyoyafanyia uamuzi, hali kadhalika hotuba zake kueleza msimamo aliyonayo, kuhusu kile Tanzania inapaswa ifanyiwe.

Pia, katika hilo ni jana tu alitoa hotuba ndefu kwa umma wa Watanzania, baada ya kuaapisha viongozi waandamizi wa kiserikali walioteuliwa kwa nafasi mbalimbali.

Sambamba na hili, amewaanikia viongozi kwamba hali ya kupanga vyema safu ya utendaji katika maeneo ya kimkoa, bado anaendelea katika maeneo mengine muhimu kwa utendaji.

Hapo alianika namna anavyotaka serikali yake itumike katika kila sekta, pia wizara zake, akiainisha kila moja anavyohitaji iwe.

Ili kupata tathmini ya awali, Nipashe iligonga hodi nyumbani kwa mwanasiasa mwandamizi na sehemu ya wazee wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mwanza, pia mdau kitaifa, Mzee Charles Masalakulangwa.

Anaanza kumtambulisha kwamba, Rais Samia amewaonyesha Watanzania uwezo mkubwa wa kuliongoza Taifa katika kile mzee huyo amekiita 'umakini bila kutokuyumba.'

Gwiji huyo wa siasa, anatafsiri haiba ya Rais kuwa na mpole, lakini ana kauli zilizojaa busara, msimamo na anachokiita "uangalifu mwingi wa kutosha kusimamia nchi," hali inayowapa matumaini watendaji watakaotaka kumwangusha katika kuchapa kazi, wakiwamo wanaokiuka nidhamu na maadili ya utumishi wa umma.

"Rais Samia anatakiwa kuwa mkali, hasa kwa mawaziri wapya aliowateua na aliowabadilisha wizara, anapoona wanakwenda tofauti na serikali yake," anasema Mzee Masalakulangwa.

KAZI KWA BIDII

Pia, anakumbusha kuwapo waliozoea kufanya kazi kwa kusimamiwa na kusukumwa ndipo ionekane bidii, anawataka kubadiika ili kumsaidia Rais kuchapa kazi, badala ya kuwachelewesha wananchi na taifa kufikia malengo yenye mafaniko ya kiuchumi.

Anaeleza imani yake kwamba, kiongozi huyo wa sasa yuko sambamba na kasi ya utendaji za mtangulizi wake, akimpa wasifu wa ujasiri, weledi na uzoefu wa kutosha, tafsiri walionayo ya matumaini Watanzania wanayo kwake.

Mzee Masalakulangwa, anataja umuhimu katika usimamizi wa miradi kama afya, maji, kilimo, ujenzi wa stendi za mabasi mikoani na masoko makuu yasiyokamilika.

"Mambo matatu anayotakiwa kuyakamilisha, kuyatekeleza ni miradi mikubwa ambayo ni ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere, reli ya kisasa(SGR) pamoja na ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi," anasisitiza Mzee Masalakulangwa...

...mini na kuleta mabadiliko kiuchumi.

Pia mwanasiasa huyo anatoa angalizo kwa serikali na chama tawala CCM, kuwa makini na aina yoyote ya dhana ya makundi, kwani kuwa nayo ni ushindi

UCHUMI NA KODI

Pia Masalakulangwa anafafanua kwamba, serikali inatakiwa kutilia mkazo suala la kilimo, ufufuaji na ujenzi wa viwanda, ili kukuza uchumi wa nchi, kwa sababu uzalishaji mkubwa wa malighafi unatokana na sekta ya kilimo.

Aidha sekta ya kilimo ndiyo yenye ajira kubwa kwa wananchi wa kawaida, ikikadiriwa kuwa asilimia 80 ya Watanzania hufanya shughuli za kilimo, biashara na ufugaji.

Mzee Masalakulangwa anasema, lakini licha kilimo kuwa pacha wa viwanda, bado serikali inakabiliwa na ugumu wa kushindwa kufikia malengo mazuri ya kujenga viwanda au kufufua vya zamani ambavyo vilikufa tangu enzi za utawala wa awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Nyerere.

Akitoa mfano wa kiwanda kilichopo jijini Mwanza cha kutengeneza nguo maarufu Mwatex, ambacho kilifufuliwa na mwekezaji na kuanza kuzalisha nguo, anakiri haijafikia rekodi ya zama hizo.

Kwa mujibu wa mwanasiasa huyo, mwenyeji wa Mwanza, Mwatex ya wakati huo ilishaweka historia ya kuajiri zaidi ya wafanyakazi 4,000, mbali na idadi kub...

UKURASA 11


# NURU MPYA

• **Rais** aagiza vyombo vya habari vilivyofungiwa vifunguliwe, apiga marufuku ubabe ukusanyaji kodi, afichua utoroshaji madini Mirerani...*Uk. 2,3 na 4*






**Bima ya Afya:**
"Watanzania wanakatwa bima ya afya wakifika kule dawa hakuna, kaliangalieni hili..."



**Mkongo wa Taifa:**
"Ile ni amana yetu, ilindwe na ilindwe vizuri sana, usalama wetu uko wapi kama kila mtu atakuja na kulaza mkongo wake"



**Uwekezaji:**
"Makampuni yanafungwa sio uongo kutokana na kero wanazo kutana nazo wawekezaji, waacheni wafurahie"



**Covid-19:**
"Suala la Covid-19, nakusudia niunde kamati ya watalaam kuangalia kwa upana wake kitaalam halafu watashauri serikali..."



**Madini:**
"Madini na kodi imekuwa vikwazo vya maendeleo kwa watumishi kukaa na kubishana na wawekezaji"



**Bandari:**
"Natoa miezi sita ntaangalia hali ya bandari inavyokwenda, halafu tutakuja kuzungumza baadaye"



**Ardhi:**
"Watu wameporwa sana ardhi zao na wanaohusika kwenye uporaji ni maofisa ardhi..."



**Kodi:**
"Matumizi ya ubabe na mabavu kwenye ukusanyaji kodi hausaidii, muende mkakusanye kodi lakini kodi za dhuluma hapana"




**Habari:**
"Nasikia kuna vyombo vya habari mlivifungia, vifungulieni lakini wafuate sheria na miongozo ya serikali na kanuni ziwe wazi"

**MICHEZO** KOMBE FA Z'BAR BAADA YA RAMADHANI UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Pangua pangua Ma-RC, ma-DED

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema pangua pangua ya wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali nchini inanukia ili kukamilisha muundo wa serikali yake.

Bila kusema lini itafanyika, ni mwendelezo wa uteuzi alioanza nao tangu Machi 31, kwa kufanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri na Aprili 4, mwaka huu, kuteua makatibu wakuu, na naibu makatibu wakuu na wakuu wa taasisi na idara za serikali.

Akizungumza jana Ikulu, jijini Dar es Salaam, baada ya kuwaapisha viongozi hao ambao baadhi ni wapya na waliobadilishwa maeneo ya kazi, alisema hivi karibuni atafanya kwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi ili safu itimie.

Aliyasema hayo wakati akichambua Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iliyo chini ya Waziri Ummy Mwalimu, ambayo aliiagiza kuhakikisha matumizi yanafanywa kulingana na sheria na kanuni.

"Nimemleta mwana mama madhubuti nimempa Katibu Mkuu mzuri na wasaidizi wake, ni imani yangu kazi itafanywa TAMISEMI ambapo ni pamoja na wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi na hiyo kazi itafuata hivi karibuni, ili safu itimie," alisema.

Pia, Rais Samia alisema TAMISEMI ina jukumu la elimu na afya za Watanzania na kuagiza waendelee na ujenzi wa miundombinu yake ili wananchi wapate fursa zaidi. Katika sekta ya elimu, aliagiza wakasimamie ujenzi wa shule za sekondari 26 za wasichana hadi ifikapo mwaka 2025 ambazo zimetengewa bajeti maalum.

Kadhalika, aliagiza TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora wakawarudishe walimu 6,000 haraka ili wakatoe huduma kwa wananchi. "Natambua kwamba kuna walimu wengi karibu 6,000 au zaidi wameacha kazi au wamestaafu, wamefariki kwa sababu mbalimbali na kunahitajika warudishiwe, hawa ni wale ambao siyo ajira mpya ni wa kufidia," alisema.

Katika afya, aliiagiza TAMISEMI iendelee kujenga hospitali za wilaya, vituo vya afya na kumalizia maboma ya zahanati. "Zipo ajira mpya za madaktari, bajeti ya mwaka huu ni kuweka vifaa kwenye vituo na hospitali zote na kuweka watumishi mkaliangalie hili," aliagiza.

Kuhusu barabara za vijijini, Rais aliagiza TAMISEMI na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kuhakikisha zinafanyiwa marekebisho kabla ya mvua.



Rais Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Alphayo Japani Kidata, kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Nuru mpya yaonekana

**Na Romana Mallya**

WATANZANIA wamezidi kuona nuru mpya na unafuu wa maisha katika serikali ya sasa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Hatua hiyo inatokana na mambo yaliyomo katika hotuba yake jana ambayo yalibainisha kuwa anapenda haki itendeke kwa kila Mtanzania na kubwa zaidi waliopewa dhamana ya kukusanya kodi wafanye bila kuwaumiza watu.

Licha ya jambo hilo, suala la uhuru wa vyombo vya habari, ambalo limekuwa lililalamikiwa kwa muda mrefu, linaonekana kupatiwa ufumbuzi baada ya kuagiza vyombo vilivyofungiwa vifunguliwe mara moja. Vilevile amezitaka mamlaka zinazosimamia vyombo vya habari kuacha kutumia nguvu na ubabe.

Akizungumza baada ya kuwaapisha makatibu wakuu, manaibu wao na wakuu wa taasisi za serikali, Dar es Salaam jana, Rais alichambua wizara na taasisi za umma moja baada ya nyingine.

Sambamba na kuzichambua, alitoboa siri wateule 49 kati ya majina 500 yaliyofikа mezani kwake na kuonyesha kiasi gani ana matumaini makubwa juu yao na kuwataka kuwatumikia Watanzania kwa uaminifu.

Pia alitumia nafasi hiyo kutoa maelekezo ya kila sekta juu ya kinachopaswa kufanyika kabla ya 2025 huku akiahidi kuwa na kikao cha kila sekta ambazo zitawajibika kuja na mipango na mikakati ya kuwatumikia Watanzania na kufikia lengo la maendeleo.

Rais Samia aliwaambia wateule hao aliowateua Aprili 4, mwaka huu, wakawatumikie wananchi bila ubaguzi na kwamba anawategemea katika kusukuma gurudumu kwa sababu wao ndio injini na mawaziri ni wanasiasa.

"Mkawatumikie Watanzania bila ubaguzi, mkawe msaada na siyo bugudha au adha, mkawe neema na siyo kero na nuksi kwa Watanzania, mkasimamie haki na si udhalimu au dhuluma na unyanyasaji. Hii ndiyo kazi yenu nawatuma kwenda kuifanya," alisema.

"Ninawapongeza kwa kujiaminisha, msingejiaminisha nisingewaamini na hatimaye mkapata uteuzi huu mlioupata leo (jana) katika nafasi mbalimbali.

"Watanzania tunakaribia milioni 60 na katika hao zaidi ya 5,000 walikuwa na sifa za kukaa pale mlipokaa nyie lakini Mungu alielekeza nyie ndio mkae hapo leo," alisema.

Hafla ya kuapishwa kwa viongozi hao, ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango; Waziri Mkuu Kassim Majaliwa; Spika wa Bunge, Job Ndugai; Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma; Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga; mawaziri na naibu mawaziri na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

# Jopo la wataalam kuishauri serikali kuhusu corona

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inakusudia kuunda jopo la wataalam kutathmini na kushauri suala la corona juu ya nini cha kufanya kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa.

Rais Samia Suluhu Hassan aliyasema hayo jana Ikulu, Dar es Salaam baada ya kuwaapisha makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na wakuu wa taasisi na idara za serikali aliowateua Jumapili.

"Ninakusudia kuunda kamati ya wataalam waliangalie suala la corona kwa upana wake na waangalie remedies (tiba lishe) kwa upana wake kitaalam halafu watushauri serikali.

"Halifai kulinyamazia ama kulikataa au kulikubali bila kufanya utafiti wa kitaalam. Tutafanya utafiti wa kitaalam, tutaunda timu ya watalaam, watuambie upeo wa suala au tatizo hili lilivyo na hayo yanayopendekezwa na ulimwengu kuja kwetu, je, yakoje kitaalam kwa utaalam wetu wa ndani," alisema huku akisisitiza kuwa anakusudia kufanya hivyo kwenye upande wa ugonjwa wa corona kwa sababu kama nchi haiwezi kujitenga kama kisiwa.

"Hatuwezi kujitenga kama kisiwa na hatuwezi kupokea yanayoletwa bila kuweka cha kwetu, bila kufanya utafiti wa kwetu, Rais (Jakaya) Kikwete (Rais wa awamu ya nne) alituambia akili za kuambiwa....eeh tuweke na zetu.

"Tuwe na msimamo maalum unaoeleweka si tunasoma mambo ya COVID-19 ulimwenguni, Tanzania deshi deshi deshi haieleweki, tueleweke kama tunakubali, tunakataa, tunafanyaje, tueleweke changanya na zako," alisema.

Machi 16, mwaka jana, Tanzania ilithibitisha mgonjwa wa kwanza wa corona mwanamke jijini Arusha ambaye aliwasili nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Ubelgiji kwa ndege ya Shirika la Rwanda.

Msafiri huyo, raia wa Tanzania, aliondoka nchini Machi 3, mwaka jana, na kati ya tarehe 5 na 13 alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena Ubelgiji.

Siku iliyofuata, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kufunga shule zote za awali, msingi na sekondari hadi kidato cha sita na baadaye vyuo vya elimu ya juu na vile vya ufundi kwa iku 30 ambazo ziliongezwa kutokana na corona.

Hadi Aprili 18, mwaka jana, wagonjwa waliogundulika Tanzania walifikia 147 huku watano kati yao wakipoteza maisha na siku hiyo Shirika la Afya Duniani (WHO) liliutangaza ugonjwa corona kuwa ni baa la dunia.

Wakati WHO ikitangaza hivyo, idadi ya wagonjwa wa corona duniani ilikuwa 2,258,909 na vifo vilifikia 154,388 huku Marekani, Italia, Hispania na Uingereza zilitajwa kuongoza kwa idadi ya wagonjwa na vifo.

Katika mlipuko huo wa kwanza wa corona, Tanzania ilifikia idadi ya wagonjwa 509 na vifo vilikuwa 21 na wagonjwa waliopona walikuwa 183.

Miongoni mwa hatua zilizochukua wakati huo zilikuwa pamoja na wananchi kuelimishwa umuhimu wa kunawa mikono, kutumia vitakasa mikono na kunawa na maji tiririka na kuzingatia umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu.

Pia wananchi katika kukabiliana na ugonjwa huo walitakiwa kujifukiza na kula vitu vya kuongeza kinga mwilini.

Wakati nchi mbalimbali duniani zikiwataka watu wake wajifungie na kufunga mipaka yao, Tanzania haikufanya hivyo badala yake kwa wageni waliokuwa wakiingia nchini walikaa karantini kwa siku 14 na wananchi waliendelea na shughuli za kiuchumi.

Mei 21, Rais John Magufuli, alitangaza kuanzia mwezi uliofuata (Juni), vyuo vyote pamoja na kidato cha sita vifunguliwe.

Mwishoni mwa mwaka jana, WHO ilitangaza mlipuko wa pili wa corona duniani na Tanzania iliendelea kusisitiza wananchi wake kuchukua tahadhari na kuendelea kufanya kazi. Sambamba na hilo, ilisisitiza kwamba ugonjwa huo haupo bali kuna magonjwa ya kushindwa kupumua.

## HABARI KITAIFA

# PSSSF hali ni mbaya kifedha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

RAIS Samia amesema hali ya kifedha ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) hivi sasa ni mbaya.

Mkuu huyo wa nchi alitoa kauli hiyo jana Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya kuwaapisha viongozi mbalimbali aliowateua usiku wa kuamkia juzi.

"Ninajua hali ya PSSSF kuwa mfuko huu una hali mbaya na ndiyo maana sikuteua mtu. Hapa tuna kazi ya kufanya kwanza kuunusuru mfuko ule halafu ndiyo tujue sasa safu ipi ya kushika huo mfuko," alisema.

Mfuko huo ni zao la kuunganishwa kwa mifuko mitatu ya hifadhi ya jamii ambayo ni PSPF, PPF na LAPF.

Kibarua Bosi TPA

Katika hatua nyingine, Rais Samia ametoa muda wa miezi sita kwa Mkurungenzi Mkuu mpya wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Erick Benedict, kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utendaji wa mamlaka hiyo.

Katika hotuba yake ya jana, Rais Samia pia aliweka wazi jinsi bosi huyo mpya wa bandari alivyokumbana na misukosuko ya kiutendaji.

"Erick ulikuwa Dar es Salaam lakini kwa sababu moja au nyingine ukatupwa Mwanza, hukuvunjika moyo, ulifanya kazi Mwanza na Mwanza umefanya kazi nzuri sana," Rais Samia alisifu.

Alisema kuwa baada ya kuona ubadhirifu na yaliyokuwa yanaendelea TPA, akaona amtoe Mwanza ampeleke Dar es Salaam na ana imani kazi aliyofanya Mwanza, kwenye eneo lake jipya la kazi ataifanya mara mbili yake

"Nenda pale usiangalie mtu usoni, ninajua ndani ya bandari kuna makundi mawili, nenda pale kafanye kazi, usimwonee mtu, Rais Samia aliagiza.



Makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na wakuu wa taasisi mbalimbali, wakila kiapo cha Maadili ya Utumishi wa Umma, baada ya kuapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Rais Afichua madini kutoroshwa Mirerani

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Saluhu Hassan, amesema uwapo wa ukuta na ulinzi mkali katika mgodi wa madini Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, havijasaidia kutunza rasilimali hiyo na sasa bado kuna utoroshwaji mkubwa.

Pia amewaagiza wizara na wataalamu mbalimbali kutotumia misuli na badala yake kufuatilia njia zinazotumika kutorosha na kutaka kutokuguswa kwa kitalu C ambacho kilishaanza kugawanywa.

Samia alitoa agizo hilo jana Ikulu, Dar es Salaam, baada ya kuwapisha makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na wakuu wa taasisi aliowateua hivi karibuni.

"Mirerani tuongeze ulinzi na ulinzi wa pale si wa kutumia mabunduki ya CDF (Mkuu wa Majeshi). Mnajua wenyewe jinsi ya kuwalinda wachimbaji wenu wasitoroshe," alisema.

Alisema CDF wanalinda juu lakini watu wanatorosha kupitia chini ya ardhi na kutokea sehemu nyingine na madini makubwa yakipatikana yanaoneshwa na serikali lakini kuna mengine ambayo bado yanatoroshwa.

Kwa mujibu wa Rais, Mirerani kuna kitalu C ambacho kimewekwa akiba lakini kwa sasa kimeanza kuvamiwa, hivyo na aliagiza kuwa walioanza kugawana eneo hilo waache.

"Kitalu hicho kina matumizi yake, hivyo sitaki kuona mkono wa mtu na walioanza kugawa maeneo katika eneo hilo waache na idara husika mkalisimamie.

"Madini yetu haya ndiyo tegemeo la nchi kwa hiyo tusipoyasimamia vizuri tunaangusha wenyewe uchumi wetu na wizara mnafanya vizuri mnaongeza fedha lakini mngeongeza usimamizi mzuri fedha hizo zingeongezeka na pengine tungekuwa wa kwanza katika soko la kimataifa kutoka nafasi ya tatu tuliyopo," alisema.

Pia alisema katika suala la ubia na kampuni za nje ikiwemo Barrick kupitia Twiga na LZ Nickel, changamoto ni nyingi ikiwamo kodi, hivyo akaagiza idara husika kushuhulikia katizo hilo.

"Hili linawagusa hadi Wizara ya Fedha. kama kuna kodi ambazo hamuwezi kusamehe katika ngazi yenu, pandisheni juu serikali ikae tujadiliane za kusamehe tusamehe lakini twende mbele.

"Lakini pia makubaliano mengine tuliongia na kampuni ya LZ Nickel na mengine nyoosheni yamalizike haraka watu wachimbe tunahitaji hiyo fedha," alisema.

Aliongeza kuwa madini hayo yakiendelea kukaa ardhini watajivunia nayo na kutaja idadi iliyopo lakini yakichimbwa yatalinufaisha taifa, hivyo wizara husika ikamilishe makubaliano ili kazi ianze kufanyika na nchi ifaidike na rasilimali hizo.

"Kama kuna matatizo ya kisera na kisheria semeni na leteni tukae tuyamalize ili mambo yaendelee," alisema.

# Bodi ya TASAC vikao 23 mwaka yatumia mil. 600/-

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amebainisha kukerwa na Bodi ya Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) kufanya vikao zaidi ya 20 kwa mwaka na kutumia zaidi ya Sh. milioni 600 kugharamia vikao hivyo.

Alifichua ulaji huo wa mamilioni ya shilingi jana mara baada ya kuwaapisha, viongozi aliowateua kushika nafasi mbalimbali, hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Saalam.

Akitoa maagizo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Kaimu Mkeyenge, Rais Samia alimtaka kwenda kulisimamia shirika hilo ili kufanya kazi zake kwa ufanisi.

"Katika jambo ambalo mmelifanya na limenikera sana, kitendo hiki ambacho mmekifanya ndani ya mwaka mmoja bodi imefanya vikao 23, na mmetumia zaidi ya Sh. milioni 600," alisema

Rais Samia alisema pamoja na bodi hiyo kufanya vikao zaidi ya 23, kulikuwa na vikao vingine ambavyo kiuhalisia ni bodi hiyo hiyo ilijigeuza kuwa kamati ndogo ndani ya shirika hilo. Alisema amebaini vikao vya kamati ndogo vilifanyika mara 11 na zaidi ya Sh. bilioni moja zimetumika katika vikao hivyo na vya bodi.

"Ulikuwa humu, nimekuinua. Sasa, nenda mkanyooshane wenyewe ndani ya shirika, ninataka shirika lifaidishe serikali, siyo lenyewe kuwa sehemu ya kutumia fedha za serikali.

"Ukiangalia kilichozungumzwa na kilichotoka ndani ya hiyo bodi, 'impact' hakuna na hapa ninataka nitumie msemo wa (Jumaa) Aweso, wewe ni kijana na mimi ni mama, ukinizingua, tutazinguana.

"Ninataka uende ukafanye kazi siyo kwenda kuinua mabega kwa wale uliowaacha pale. Kama mna makundi yenu, nenda ukayamalize, tunataka TASAC izalishe na siyo yenyewe kutumia," aliagiza.

Pia, alisema kuwa pamoja na Bodi, hiyo kukaa vikao hivyo lakini hakuna kitu ambacho kilijadiliwa kuwa na tija kwa shirika hilo.

# Rais atoa mwanga uhuru wa habari

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza kufunguliwa kwa vyombo vyote vya habari ambavyo vilikuwa vimefungiwa.

Sambamba na kufunguliwa, ameagiza wasimamizi serikalini kuacha ubabe dhidi ya vyombo hivyo.

Rais Samia alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam baada ya kuwaapisha makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali. Bila kuvitaja idadi na majina, aliagiza kufunguliwa kwa vyombo hivyo na vijiendeshe kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi.

Pia aliagiza kanuni za adhabu zinazotumika kuvichukulia hatua vyombo vya habari kupitiwa upya ili kuweka uwazi na adhabu zichukuliwe kulingana na kanuni zilizowekwa badala ya kutumia ubabe.

"Kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.....mmhhh...? huku nina mengi. Lakini ni kusimamia vyombo vya vyetu vya habari vya ndani.

"Nasikia kuna vijivyombo vya habari huko mlivifungia fungia, sijui viji TV vya mikononi vile. Vifungulieni lakini wafuate sheria na miongozo ya serikali. Vifungulieni tusiwape mdomo wa kusema tunaminya uhuru wa vyombo vya habari.

"Lakini mhakikishe kila mliyempa ruhusa ya kuendelea na chombo cha habari anafuata sheria za serikali na kanuni ziwe wazi. Kosa hili adhabu yake ni hii na mnakwenda kwa adhabu mlizoziweka kwenye kanuni. Tusifungie tu kibabe, wafungulieni lakini tuhakikishe wanafuata kanuni na miongozo ya serikali."



Rais Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Emannuel Tutuba, kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wadau wa habari kicheko kila kona

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa habari nchini wamepokea kwa shangwe agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuitaka Wizara ya Habari kuvifungulia vyombo vya habari vilivyofungiwa, huku wakisema kuna tumaini kubwa katika tasnia hiyo.

Wadau hao kwa nyakati tofauti walisema wamepokea kauli hiyo kwa shangwe na wanaamini ni ukombozi na mwanzo mzuri wa uhuru wa vyombo hivyo ambao ulikosekana kwa kipindi kirefu.

Walisema kauli hiyo imeleta matumaini mapya kwa tasnia hiyo ambayo yalianza kufifia na kumuomba aangalie upya sheria kandamizi zinazotumika kuviadhibu vyombo hivyo.

**MISA-TAN**

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-Tan), Salome Kitomari, amempongeza Rais Samia kwa kuweka tumaini jipya kwa tasnia ya habari ambayo ilikuwa katika mtanziko mkubwa, huku kukiwa na idadi kubwa ya wahariri na waandishi wazuri wasio na kazi kutokana na kudumaa kwa vyombo hivyo.

"Siku zote taifa lisilo ongea ni taifa mfu, nasi tulikuwa tunaelekea huko, uhuru wa vyombo vya habari siyo idadi ya magazeti, TV au radio bali vinavyotekeleza wajibu wake kwa msingi ya kuburudisha, kuelimisha na kukosoa pasipo kuingilia na mamlaka yoyote, bali kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi," alisema.

Kwa mujibu wa Kitomari, tumaini jipya limekuja ikiwa Mei 3, mwaka huu ni maadhimisho ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari, ambayo huadhimishwa kila mwaka, na kwa kutambua mchango wa vyombo hivyo kama muhimili wa nne usio rasmi sasa vitazidi kukua na kulisaidia taifa kimaendeleo.

**MCT**

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, alimpongeza Rais Samia kwa uamuzi huo na kusema jambo hilo lilikuwa linatia doa nchi kimataifa.

Alisema wanaamini kwamba huo ni mwanzo mzuri kwa nchi na wanatumaini wizara husika italifanyia kazi kwa haraka agizo hilo.

"Tutambue kwamba miongoni mwa mambo ambayo yamekuwa yakichangia vyombo vingi vya habari kufungiwa ni pamoja na uwapo wa sheria mbovu zinazoendesha vyombo hivyo, kwa hiyo hizi nazo zinatakiwa kuangaliwa upya kwa sababu pasipo kufanya hivyo vitaendelea kufungiwa," alisema Mukajanga.

**TEF**

Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), kwa upande wamemepokea kwa furaha maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia ya kutolewa kifungoni kwa vyombo vya habari ambavyo vimekuwa katika kifungo.

"Hili litasaidia ikiwa chombo husika hakikuridhika na adhabu, kukata rufaa kwa mujibu wa sheria. Ikumbukwe kwamba hatua ya Rais imekuja wakati ambao baadhi ya vyombo vya babari nchini yakiwamo baadhi ya magazeti na vile vya mtandaoni vikiwa vimefungiwa kwa muda mrefu na baadhi yake kufutwa, licha ya kushinda rufaa katika mamlaka za kisheria," alisema Kaimu Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile. TEF pia wamemkaribisha Mkurugenzi mpya wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa na kwamba wako tayari kumpa ushirikiano utakaowezesha kukua kwa sekta hiyo.

**MOAT**

Kaimu Mwenyekiti wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), Samwel Nyala, alisema kauli ya Rais Samia ni mwanzo mwema na mapatano mazuri kwa vyombo hivyo vya habari.

**TADIO**

Mwenyekiti wa Mtandao wa Radio za Kijamii Tanzania (TADIO), Prosper Kwigize, alisema kauli hiyo ya Rais Samia ni dalili njema ya ukombozi kwa vyombo vya habari nchini na ametambua mchango wa vyombo hivyo kwa taifa.

Alisema jambo la msingi kwa sasa ni serikali kukaa na wadau wa vyombo hivyo, kujadili upungufu uliyopo katika sheria na kanuni zinazosimamia habari ili kuondoa matatizo ambayo yamekuwa yakichangia vyombo hivyo vya habari kufungiwa.

**TAMWA**

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe, alisema kauli ya Rais Samia imeleta faraja kwa wanahabari.

**UPTC**

Rais wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UPTC), Deogratius Nsokolo, alisema ni mwanzo mzuri ambao Rais ameuanza katika kurejesha uhuru wa vyombo vya habari nchini.

**JOWUTA**

Kwa upande wa Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania (JOWUTA), Katibu wa chama hicho, Selemani Msuya, amesema kimepokea kwa furaha na matumaini kauli ya Rais Samia na kwamba wanamini huo utakuwa msaada mkubwa kwa waandishi wa habari hususani vijana ambao wengi wao walikosa kazi baada ya vyombo vyao kufungiwa.

# TRA yapigwa 'stop' kutumia nguvu kudai kodi

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeagizwa kuacha matumizi ya nguvu na ubabe katika ukusanyaji wa kodi kwa sababu haisaidii.

Alitoa agizo hilo jana Ikulu jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa suala hilo husaidia kwa muda mfupi tu.

"Nimepewa takwimu za vikosi kazi mnavyounda namna mlivyokusanya lakini si endelevu kwa sababu mtakwenda mtamminya mtu, mtamkamua mtu mtakusanya leo mlichotaka.

"Mtamtisha na kumpiga uhujumu uchumi anaogopa kwenda jela, atajikwangua atalipa lakini unaua biashara yake, anaifunga, kesho na kesho kutwa nani atakulipa hiyo kodi kwani lazima muue?" alihoji Rais samia Suluhu Hasssan, jana.

Alisema kinachomshangaza ni wale watu wanaowapigia miaka mitano au 10 nyuma anakwenda na cheti cha kulipa kodi TRA lakini anaambiwa alikiuka hiki au kile alipe.

"Alipokiuka hiki wewe ulikuwa wapi? Kama alikiuka kwa nini ulimpa cheti cha kulipa kodi? Leo unamrudia unampigia kodi tele za nyuma aje alipe, anashindwa anafunga biashara anaogopa kwenda jela. Ninaomba mkatizame hili, kodi alipe lakini kodi za dhuruma hapana, kwa sababu hazitatufikisha mbali," alisema.

**MAMBO YA NJE**

Aliitaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhakikisha wanakuza uhusiano na nchi za nje na kumweleza Waziri wake, kuwa anafahamu ni hodari kwenye hilo ndiyo maana amemrudisha kwa sababu wanamsikiliza na ni hodari.

"Nimemuweka mama shupavu na madhubuti anayeijua wizara nje, ndani, lakini kuna katibu mkuu anayejua wizara vizuri ninajua umeshakaa nje kutuwakilisha, leo ni Katibu Mkuu, nitakusaidia kazi moja ya Mkuu wa Itifaki, naomba tusadiane kumtafuta, ili ujikite kwenye kazi yake," alisema.

"Kuna msemo ukitaka kufika mbali nenda na wenzako lakini ukitaka kufika haraka nenda peke yako, unafika haraka je, unafika na lengo ulilokusudia? Hatutaki kwenda peke yetu, twende na wenzetu, mkarekebishe hayo," aliagiza.

Aonya miungu watu

Katika hatua nyingine, Rais Samia aliwaonya wanaosimamia vibali vya kazi kuwa waungu watu na kugeuza kazi hiyo kuwa mradi wa kuchuma fedha na kuagiza suala hilo likasimamiwe.

Alisema kuwapo kwa mazingira hayo kumesababisha wawekezaji kufunga kampuni zao na kuondoka.

Aliagiza wahusika wakasimamie suala hilo kwa weledi kwa sababu mwekezaji anapotaka kibali cha kazi anazungushwa mpaka akikipata inakuwa imeshamtoka Dola 10,000 au 8,000 au Dola 5,000.

# SMZ yazuia bil. 4.79/- za kampuni ya upatu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imezuia jumla ya Sh. bilioni 4.79 kutoka kwa mmiliki wa Kampuni ya Masterlife Microfinance, ambayo ilikuwa ikiendesha biashara ya kifedha kinyume cha sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kufungiwa kwa kampuni hiyo, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema kuwa kupitia biashara hiyo imeleta mtafaruku mkubwa ikizingatiwa kwamba hadi sasa imeshapokea Sh. bilioni 38.50 ambazo ni fedha za wananchi 39,000.

Alisema tangu serikali kuifungia kampuni hiyo Machi 4 mwaka huu, anafahamu kuwa imeleta taharuki katika nchi kwa vile wananchi walikuwa na matumaini makubwa na biashara hiyo, na baadhi yao wakiwa wamejiunga na kampuni hiyo kwa kuchukua mikopo mikubwa kutoka kwenye benki.

"Naomba nieeleze kwa muhtasari, kampuni hii inatuhumiwa kutokuwa na vibali halali kisheria katika utekelezaji wa shughuli ambazo walikuwa wanazitekeleza, kwa maana ya kwamba kupokea fedha kutoka kwa wananchi," alisema.

Alieleza kuwa serikali inafahamu machungu na taharuki iliyopo kwa wananchi juu ya suala hilo, kwa hivyo jambo hilo sasa linashughulikiwa na vyombo vya sheria.

Dk. Mwinyi alieleza kuwa kampuni hiyo ilitumia nyaraka za usajili uliofanywa Tanzania Bara na Wakala wa Usajili wa Biashara na Lesseni (BRELA) na kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania Julai, 2020 ambapo iliwekwa katika daraja la walipa kodi wadogo na ikajihusisha na biashara ya kufuga wanyama pamoja na kutengeneza na kusindika vyakula.

Alisema ni jambo la kushangaza sana kuona kwamba kampuni hiyo haikutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa usajili, badala yake imekuwa ikijihusisha na biashara ya kukusanya fedha kutoka kwa wananchi.

# Askofu Maluma afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU wa Jimbo Katoliki la Njombe, Alfred Maluma, amefariki dunia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu.

Taarifa ya kifo cha Askofu Maluma zilitolewa jana na Padri Justin Sapula wa jimbo hilo, akieleza kuwa kilitokea usiku wa kuamkia jana saa 6:40 usiku katika hospitali hiyo.

Katika taarifa hiyo, Padri Sapula alisema: "Taratibu za mazishi zinaendelea kufanyika, mtapewa taarifa kwa wakati, astarehe kwa amani Baba Mhashamu Alfred Leonhard Maluma."

Kadhalika, taarifa hiyo ilieleza kwamba: "Taarifa ziwafikie Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania- Askofu Mkuu, Gervas Nyaisonga, Balozi wa Baba Mtakatifu nchini, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, maaskofu wakuu, maaskofu, mapadri, watawa wa kike na kiume, waumini walei Jimbo Katoliki Njombe, ndugu wa familia, mapadri, watawa wote wa Kanisa la Tanzania.

# Mgombea CCM Muhambwe ampinga wa ACT-Wazalendo

**Na Deogratius Nsokolo,** KIBONDO

MGOMBEA wa Chama Cha Mapinduzi CCM, Jimbo la Muhambwe wilayani Kibondo, Dk. Florence Samizi, amekata rufani dhidi ya mgombea wa Chama cha ACT Wazalendo, Julius Masabo, baada ya pingamizi lake la awali kutupwa na msimamizi wa uchaguzi katika jimbo hilo.

Msimamizi wa uchaguzi katika Jimbo la Muhambwe, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, Diocles Lutema, alisema Masabo amekatiwa rufani ndani ya muda baada ya pingamizi la awali kutupwa na uamuzi wa rufani hiyo utafanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Alitaja sababu za rufani kuwa ni pamoja na madai ya wadhamini wa Masabo kulazimishwa na saini zao zina walakini na madai mengine ni kuwa picha za mgombea huyo wa ACT - Wazalendo hazijakidhi vigezo kwa mujibu wa sheria.

Lutema alisema pamoja na rufani hiyo wagombea wote watatu walioptishwa wanaendelea na kampeni na tayari ratiba imekwishapangwa kwa ushirikiano wa vyama vyote vya siasa vinavyogombea katika uchaguzi huo wa kujaza nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, marehemu Atashasta Nditiye. Wagombea katika uchaguzi huo utakaofanyika mei pili mwaka huu, ni Dk Florence Samizi wa Chama cha Mapinduzi, Julius Masabo wa ACT- Wazalendo na Philipo Fumbo wa Democratic Party (DP).

Pia msimamizi huyo wa uchaguzi amewataka wagombea kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kampeni ili uwe wa amani na utulivu na kwamba maandalizi yanaendelea vizuri.

Alisema zaidi ya wapiga kura 127,000 walio kwenye daftari la kudumu la wapiga kura wanatarajiwa kupiga kura kuchagua mbunge wa Jimbo la Muhambwe.

Akizungumzia uchaguzi huo Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, Luis Bura, amesema wananchi wanatakiwa kuhudhuria mikutano ya kampeni ya wagombea ili kufahamu malengo ya wagombea na kwenda kupigakura siku ya uchaguzi na kwamba hali ya ulinzi na usalama katika wilaya imeimarishwa ili kuhakikisha kampeni zinafanyika vizuri. Kwa upande wao baadhi ya wananchi wameviomba vyama vya siasa vinavyogombea kufanya kampeni za kistaarabu badala ya matusi na mambo mengine yasiyo na faida kwa wananchi.


KUMBUKUMBU YA MIAKA 49




SHEIKH ABEDI AMANI KARUME

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Benki ya TPB, tunaungana na Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa **Dr Hussein Ally Mwinyi** Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar pamoja na Watanzania wote katika kumbukumbu ya miaka 49 ya kifo cha Raisi wa kwanza wa Zanzibar

Hayati Sheikh Abeid Amani Karume

www.tpbbank.co.tz info@tpbbank.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo Rais Samia uhuru wa habari

**JANA** Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa tumaini jipya kwa sekta ya habari kwa kutaka uhuru wa vyombo vya habari kuwapo nchini, kwa kufungulia vyombo vilivyopo kifungoni kwa muda mrefu na kusisitiza usimamizi wa sheria na kanuni za taaluma hiyo. Tunampongeza Rais Samia kwa kauli yake yenye matumani makubwa kwa sekta ya habari na wanahabari wenyewe, kwa kutambua kuwa taifa lisiloongea ni taifa mfu, maana yake unapozuia watu kuongea, unatengeneza taifa la hofu na huwezi kujua yanayoendelea upande wa pili.

Hili ni tumaini jipya kutokana na uhalisia kwenye vyombo vya habari kuwa kwa sasa badala ya kuajiri Watanzania, kulipa kwa wakati na kuchangia uchumi wa nchi, pamoja na kuisaidia serikali kama jicho muhimu, ilijikuta katika kufubaa kiasi cha kuelekea kushindwa kujiendesha. Kuna magazeti, vituo vya TV na redio nyingi ambavyo vipo kifungoni kwa makosa mbalimbali, na baadhi viko kwenye kifungo cha maisha, huku waliokuwa wameajiriwa wakiwa nyumbani, kushindwa kusaidia wategemezi wao na kulipa kodi za nchi.

Kauli ya Rais Samia imekuja kwa wakati sahihi, ambao Mei 3, kila mwaka vyombo vya habari vitaadhimisha siku ya uhuru wa vyombo vya habari dunia, ambao msukumo mkubwa ni kuhakikisha siyo tunakuwa na idadi kubwa ya vyombo vya habari, lakini vinavyotimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizopo.

Vyombo vya habari ni muhimili wa nne wa nchi, yaani baada ya serikali, Bunge na Mahakama, na wajibu wake mkubwa ni kuelimisha, kuburudisha, kukosoa na kutengeneza ajenda ambayo ikitekelezwa vizuri utasaidia sana serikali, kwa kuwa ni jicho lake katika mambo ambayo haiwezi kuyaona.


Vyombo vya habari vimesaidia kuibua madudu mengi ya kuisadia serikali kuchukua hatua, hivyo kuvibana vyombo vya habari kiasi cha kushindwa kujiendesha, kuajiri na mengine mengi ni kuwaumiza Watanzania. Leo hii vyombo vya habari vina idadi kubwa ya wahariri na waandishi, ambao walikuwa ndani ya vyombo vya habari, lakini wako nje ya ulingo kutokana na hali ngumu ya kiuchumi, na sasa kwa kupewa uhuru maana yake vitaweza kuibua habari mbalimbali za kuisaidia serikali pamoja na kuwasemea wanyonge. Iwapo kutakuwa na vyombo vya habari imara, vitalisaidia taifa kusonga mbele, na vitakuwa mjenzi mzuri wa taifa kwa kuwa tunaamini jicho lake ni kali, ambalo litakwenda kuona yaliyo nyuma ya pazia, ambayo yataisaidia kutafutiwa ufumbuzi. Ni muhimu viongozi wakakubali kukosolewa kwa kuwa siyo wakati wote wa kusifiwa. Ibara ya 18 ya Katiba ya Tanzania ambayo ndiyo sheria mama inasema kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake, anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila kujali mipaka ya nchi, anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake na anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi.

Wajibu huo ndiyo unavipa nguvu vyombo vya habari kutimiza wajibu wake, lakini wakati mwingine vimejikuta katika wakati mgumu. Vyombo vingi vya habari ni vya sekta binafsi na vina mchango mkubwa kwa taifa, lakini vinaposhindwa kujiendesha maana yake hata kodi kidogo vilivyokuwa vinalipa haitakuwapo, na idadi ya wasio na ajira itaongezeka.

Tunampongeza rais kwa kuona umuhimu wa uhuru wa vyombo vya habari na kutamka kuwa viachwe, inaonyesha ni muumini wa uhuru wa kujieleza.

Tunamwomba Rais Samia kutupia jicho eneo la matangazo ili kuhakikisha sekta binafsi nayo inapata matangazo kiushindani kama vilivyo vyombo vingine vya habari, na kwa kuwa wote wanachangia katika uchumi wa nchi, jambo ambalo litapunguza kama siyo kumaliza ukali wa maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Msimamo wa jana Rais Samia, kina DC na DED mjiangalie

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya mambo ambayo viongozi wa kitaifa wamekuwa wakikutana navyo wanapofanya ziara mikoani na wilayani, ni kupokewa na mabango ya wananchi yenye ujumbe wa malalamiko kero mbalimbali zinazowakabili.

Hata hivyo, wakati mwingine, kero hizo si za kitaifa kwa maana kwamba, zinaweza kumalizwa na viongozi wa maeneo husika badala ya kuziacha zisubiri viongozi wa kitaifa.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, ameamua kuja na msimamo wake kwamba, iwapo viongozi wa kitaifa wataendelea kukutana na mabango katika ziara zao, 'atawasaidia kazi' mkurugenzi wa halmashauri na wakuu wa wilaya husika.

Lakini ana agalizo katika hilo, kwamba ni pale lalamiko litakuwa ni la enero lile na si la kitaifa.

Kimsingi, msamiati 'kuwasaidia kazi' aliibua hivi karibuni ikiwa sawa na 'kutumbua', hivyo ni wazi wakurugenzi wa halmashauri na wakuu wa wilaya wamekalia kuti kavu, pale wanapolea kero za wananchi.

Ni wazi sasa kila mmoja anapaswa kutekeleza wajibu wake, ili kuweka mambo sawa. Pia, namnukuu katika onyo lingine, wananchi wanapokuwa na mabango yao wakitaka kuonyesha kwa viongozi wa kitaifa wanazuiwa, kwa lengo la kuficha ukweli usijulikane.

Haipendezi kuona watu wanakuja na mabango kuelezea kero zao, halafu watendaji wanayakusanya na kwenda kuyaficha, ili viongozi wa kitaifa wasiyasome.

Mtindo wa kuficha mabango ya wananchi, hauwezi kuwa dawa ya kumaliza kero zao, bali kinachotakiwa ni kuzishughulikia kusaidia kuwafanya waendelee kuiamini serikali yao.

Ninaamini kwamba, Watanzania wameshuhudia namna Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dk. John Magufuli, mbali na kuona mabango, alikuwa pia akikutana na baadhi ya wananchi wenye kero na kuwasikiliza.

Mara kadhaa, baadhi ya kero zilikuwa ndani ya uwezo wa viongozi wa maeneo husika, lakini cha kushangaza kuona hadi zinapelekwa kwa viongozi wa kitaifa kana kwamba wao hawapo.

Kuna wakati mwingine inawezekana baadhi ya wananchi wasijue ni wapi pa kupeleka kero zao au wamekuwa wakizungushwa tu bila mafanikio na kuona njia pekee ni kuwafuata viongozi wa ngazi ya kitaifa. Ninaamini kwamba, hayo viongozi wa maeneo husika watakuwa wanajua, lakini si vibaya wakaanzisha utaratibu wa kusikiliza kero za wananchi wao na kuwaelekeza njia sahihi ya kufanya, pale wanapokuwa na matatizo.

Kwenye jambo hili, iwapo kila mmoja atatimiza wajibu wake, hakutakuwa na mazoea ya wananchi kuendelea kusubiri viongozi wa kitaifa na kuwapokea kwa mabango yenye malalamiko mbalimbali.

Binafsi siamini kama kero zote zinazoandikwa kwenye mabango zinatakiwa kutatuliwa na viongozi wa kitaifa. Inawezekana wananchi wakawa hawaelewi mipaka au wanakwamishwa na viongozi katika maeneo yao.

Hivyo, ujumbe uliotolewa na rais kwa wakurugenzi na wakuu wa wilaya ungefaa kuchukuliwa kama mwanzo wa kujipanga upya kuhakikisha kila kiongozi anatimiza wajibu ipasavyo kwenye eneo lake la kazi.

Iwapo mwananchi ana malalamiko yaliyo juu ya uwezo wa kiongozi wake, ni vyema akaawambia na kuwaelekezwa hatua za kufuata, kwa ajili ya kupata haki, ili kumaliza mabango katika ziara za viongozi wa kitaifa.

Tayari Rais Samia, ameshajipambanua kuwa hataki kuona mtindo wa viongozi wa kitaifa wanapokewa na mabango ya yale yanayotatulika. Kilichobaki ni walengwa kuchukua hatua kuhakikisha hakuna hali kama hiyo tena.

Kwa wale waliokuwa wakifuatilia ziara za Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dk. John Magufuli, watakumbuka jinsi alivyokutana na mabango na wakati mwingine baadhi ya wananchi kulia mbele yake.

Ni hali iliyolazimisha kuwaruhusu wapande jukwaani katika mikutano ya hadhara, kuelezea kero zikiwamo za ndani ya uwezo wa viongozi wa maeneo husika na kuwaagiza wazitatue haraka iwezekanavyo.

Mtindo huo umeonekana wazi kuwa ni kero, itakuwa ni vyema iwapo kila kiongozi atatimiza wajibu ipasavyo kwenye eneo lake la utawala kuliko kusubiri kuondolewa kwenye kazi.

HABARI KITAIFA

# Neema umeme kijijini yanukia

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANANCHI wa Kijiji cha Nandambi, Kata ya Chikonji, Manispaa ya Lindi, wanatarajia kuondokana na tatizo la kuendelea kuishi gizani, baada ya serikali hiyo, kuahidi kulitatua kwa muda mfupi kwa kupeleka huduma ya umeme mwishoni mwa mwezi huu.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Shaibu Ndemanga, alipokuwa anazungumza na wakazi hao, katika mkutano wa hadhara kijijini hapo.

Ndemanga alitoa ahadi hiyo, baada ya wakazi hao kuwasilisha mbele ya yake kilio cha kukosa huduma hiyo, tangu Taifa lipate Uhuru, lakini wanaendelea kuishi gizani, huku maeneo mengine wakinufaika na huduma hiyo.

Aliwahakikishia kuwa tatizo linalowakabili la kukosa huduma hiyo, litamalizika ifikapo mwishoni mwa huu, kwa kuwa serikali inaendelea kukamilisha kupeleka umeme maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

"Ombi langu kwenu muendelee kuwa na subira, tatizo hili la kuendelea kukaa gizani litakwisha ifikapo mwishoni mwa mwezi huu," alisema Ndemanga.

Ndemanga aliwasisitiza wananchi wafanye kazi kwa bidii ili wawe na uchumi mzuri, utakaowaondoa kwenye umasikini.

Wakiwasilisha kilio hicho kwa niaba ya wanakijiji wenzake, Abdallah Mohamedi, Isumaili Yusufu na Mwabibi Yohana kwa nyakati tafauti, waliiomba serikali kuwakumbuka kwa kuwapelekea huduma ya umeme, ili waondokane na tatizo la kuendelea kuishi gizani kwa miaka mingi.



Mfanyabiashara wa machungwa akiwauzia wateja wake katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Chungwa moja linauzwa 40/- kwa bei ya jumla. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Zitto ataja sababu ACT kushiriki uchaguzi mdogo

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema wameamua kushiriki katika Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Muhambwe mkoani Kigoma ili kupima kama mabadiliko ya uongozi wa juu serikalini yanakwenda sambamba na watendaji wa ngazi za chini.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Idara ya Habari ya chama hicho, ilimnukuu Zitto akibainisha sababu za chama chao kushiriki katika uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Mei 2, mwaka huu.

"Tulipoamua kushiriki Uchaguzi Mdogo wa Muhambwe, tulitaka kuona kama kubadilika kwa Rais kunabadili tabia za watendaji. Tumevuka vikwazo viwili, moja ni uteuzi. Mkurugenzi hakukimbia ofisi tofauti na ilivyokuwa kwenye uongozi uliopita."

"Pili, pingamizi. Mkurugenzi katupilia mbali pingamizi la Chama Cha Mapinduzi (CCM). Sasa kampeni," Zitto alisema.

Uchaguzi mdogo katika Jimbo la Muhambwe umeitishwa kisheria kufuatia kifo cha aliyekuwa mbunge wake, Atashasta Nditiye, aliyefariki dunia Februari, mwaka huu mjini Dodoma wakati akipatiwa matibabu baada ya kupata ajali ya gari.

# Mwigulu awapa matumaini wafanyabiashara

**Na Benny Mwaipaja**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewahakikishia wafanyabiashara kuwa Wizara yake itahakikisha inarejesha taswira na uhusiano mzuri katika masuala ya kodi ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na kusisimua uchumi wa nchi.

Alitoa ahadi hiyo Ikulu Jijini Dar es Salaam alipozungumza na vyombo vya habari, baada ya tukio la kuapishwa kwa makatibu wakuu na naibu makatibu wakuu pamoja na viongozi wa taasisi, tukio lililofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tutatengeneza vyanzo vipya vya makusanyo ili mzigo wa kodi usibebwe na wachache kwa sababu kadri mzigo unavyobebwa na wengi ndivyo nafuu inavyopatikana, hatua itakayowafanya wafanyabiashara wengi kulipa kodi kwa hiari," alieleza Dk. Nchemba

Aidha, Dk. Nchemba aliyeanza kazi hivi karibuni kama Waziri wa Fedha na Mipango, alisema amekutana na wataalam wa Wizara yake na kuwaagiza wakutane na wenzao wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kujadili namna ya kutatua changamoto za Muungano, na kwamba anaamini zitapatiwa ufumbuzi.

"Shida ya watu wetu wengi wanapojadili masuala haya hawatuambii walipokwama, kwa hiyo niliwaambia watubainishie wanapokwama ili tupate ufumbuzi wa jambo hilo baada ya hapo tutakaa Wizara tatu, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar na Ofisi ya Makamu wa Rais na kufanya uchambuzi wa kina," alifafanua.

Kuhusu udhibiti wa matumizi wa Fedha za Umma, alisema Wizara yake itatumia mifumo ya fedha iliyobuniwa kudhibiti matumizi ya serikali na kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili iwe michache lakini yenye ufanisi pamoja na kuimarisha masuala ya utawala katika kukusanya mapato na matumizi yake ili fedha hizo zilete matokeo yaliyokusudiwa.

Waziri huyo alishuhudia kuapishwa kwa watendaji wake wapya, akiwamo Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Khatibu Kazungu.

## NMB yajivunia kupiga jeki huduma za afya

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imesema inachangia sana kuokoa maisha kwa kutoa misaada katika vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini.

Misaada hiyo imewezesha kuboreshwa kwa huduma za afya na hivyo kuwawezesha Watanzania wengi kunufaika.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Uwajibikaji kwa Jamii wa NMB, Aloyce Kikois, na kueleza kuwa misaada hiyo ni sehemu ya mpango wa uwajibikaji katika jamii wa benki hiyo wenye bajeti ya takribani Sh. bilioni moja kwa mwaka.

"Katika utekelezaji wa wajibu wetu kwa jamii, tumejikita zaidi katika maeneo matatu ya kipaumbele ambayo ni elimu, afya na huduma jumuishi za fedha na huwa tunatenga asilimia moja ya faida ya benki baada ya kodi kwa ajili hiyo.

Kila tunachokifanya huwa tunalenga kuhakikisha kinaongeza thamani kwenye jamii husika na kuonesha uendelevu wa malengo yetu," alisema Kikois.

Kwenye upande wa afya, Kikois alisema lengo kuu ni kuhakikisha vifaa tiba vipo kwa ajili ya wateja wake, wadau na jamii kwa ujumla kwa kutoa vitanda vya wodini, vitanda vya kujifungulia na vifaa vingine muhimu kwa utabibu. mKwa mujibu wa Kikois, benki hiyo iliamua kuchagua afya kama moja ya sekta ambazo zitapokea msaada kutokana na kuthamini umuhimu wa wajawazito, watoto na watu wengine wanaohudumiwa kwenye vituo hivyo na Watanzania wote kwa ujumla.

"Tunataka wateja wetu wawe na uhakika wa afya zao. Mwaka mzima tunafanya nao biashara wakiwa na afya njema, lakini wanapougua lazima wajue sisi pia tupo kwa ajili yao. Ndiyo maana tumeamua kati ya faida inayopatikana na sekta ya afya nayo ifaidike," alisema Kikois wakati maofisa wa NMB walipokuwa katika ziara ya kutembelea taasisi zilizonufaika na misaada yake katika Kanda ya Kaskazini. Katika ziara ya kanda hiyo inayojumuisha mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, maofisa wa NMB walitembelea vituo vinne kikiwemo kituo cha afya kilichopo katika Chuo cha Polisi (CCP) Moshi, Kituo cha Afya Pasua wilayani Moshi, Hospitali ya Wilaya Hai mkoani Kilimanjaro na Kituo cha Afya Oltrumet kilichopo Wilaya ya Arusha mkoani Arusha.

Katika Kituo cha Afya Pasua, Benki ya NMB imesaidia vitanda na vifaa vya kujifungulia ambapo Ofisa Muuguzi Msaidizi wa kituo hicho, Mwantumu Silayo, alitoa ushuhuda namna walivyopiga hatua baada ya kupokea msaada huo. "Hakika tulikuwa na changamoto kubwa ya vitanda vya uchunguzi na vya kulalia wagonjwa wodini. Kutoka NMB tumepokea vitanda vya kufanyia uchunguzi viwili, vitanda vya kulalia wagonjwa vitano, shuka 49 na vifaa vya kuzalishia wajawazito.

"Kwa mwezi tunapokea zaidi ya wagonjwa 150. Awali daktari alikuwa analazimika kumfanyia uchunguzi mgonjwa huku amesimama au amekaa kwenye kiti. Kimsingi mgonjwa anatakiwa alale hasa kwa wajawazito au watu wenye matatizo kwenye via vya uzazi. Kwa sasa mambo ni mazuri na hata idadi ya wajawazito wanaojifungua imeongezeka," alisema B Silayo.

Mwakilishi wa hospitali ya Oltrumet iliyopo Wilaya ya Arusha, Dk. Consolata Sweya, alisema wamepokea magodoro, shuka na vitanda vya kulalia wagonjwa.

"Msaada huu umerudisha uhai wa hospitali yetu, ndiyo maana vitanda vyote tuliamua kuvipeleka wodi ya wazazi. Hospitali hii awali ilisahauliwa lakini katika uongozi wa Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alipotembelea hapa akaagiza ifufuliwe. Kwa sasa inahudumia eneo kubwa ni kama hospitali ya wilaya.

"Kwa siku tunazalisha kati ya wajawazito 10 hadi 13, wodi ya wazazi ina vitanda 18. Lakini changamoto kubwa tuliyonayo ni vitanda vya watoto njiti. Hivyo tunaiomba NMB itufikirie katika eneo la watoto njiti," alisema Dk. Sweya.

NMB imekuwa kinara wa kuwekeza katika miradi ya kijamii kutokana na ufanisi wa shughuli zake ikiwamo kuongoza kutengeneza faida ambako huiwezesha kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili hiyo ikitumia zaidi ya Sh. bilioni 5 kati ya mwaka 2015 na 2020.

# Ugoro unavyotumika kuibia watu magari

**Na Elizabeth John**, NJOMBE

WAMILIKI wa vyombo vya moto wametakiwa kuwa makini wanapokuwa sehemu za starehe ili kuepuka kuwekewa vilevi vinavyochanganywa na ugoro na kusababisha kuibiwa magari yao.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, baada ya kukamata magari matano yaliyoibiwa sehemu mbalimbali hapa nchini.

Alisema kutokana na jitihada za jeshi hilo mpaka sasa linawashikilia watuhumiwa wawili aliowataja kuwa ni Richard Malembo, mkazi wa Msasani Dar es Salaam na Raphael Mgina, mkazi wa Miva, mkoani Njombe kutokana na kuhusika na wizi wa magari hayo.

Alisema magari yaliyoibiwa ni Noah ambayo iliibwa Madaba na Isuzu Trooper, ambazo zote wamiliki wake wamepatikana, mengine ni Toyota Carina, Toyota Premio pamoja na Canter ambazo wamiliki waliombwa kufika na nyaraka muhimu ili kuzitambua.

"Tunawasihi wananchi unapokuwa kwenye kilevi na unakuwa na mtu ambaye humfahamu angalia usalama wako kwanza na usiangalie unakunywaje na unatoka mara ngapi ukiondoka umeacha glasi ujue upo hatarini," alisema Issah.

Alisema jeshi hilo litaendelea kuyakamata magari yanayoibiwa kwa mtindo huo na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano wanapoona vitendo vya namna hiyo vikifanyika.

Aidha, Issah alisema kuna mtindo umezuka katika Mkoa wa Njombe na maeneo mengine ya nchi ambao wa watu kuingia kwenye nyumba za ibada na kuiba vifaa.

"Mbele yenu kuna spika mbili, kompyuta na mixer hivi ni vitu vya kanisa ambalo lipo hapa mkoani Njombe linaitwa glory miracle ministry vimeibiwa tarehe 31 mwezi huu vikawa haijulikani aliyeiba," alisema Issah.

Alisema kutokana na wizi wa vifaa hivyo jeshi hilo linawashikilia watuhumiwa wanne na upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Alitoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kuiba vitu vinavyotumika katika nyumba za ibada kwa kuwa ni ishara ya kukosa hofu ya Mungu.



Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, (kulia), akivuka kwenye barabara ambayo imekatwa na maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha inayounganisha vijiji viwili vya Bugwandege na Uzogore, Manispaa ya Shinyanga, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waziri ashtukia ufisadi ujenzi wa machinjio

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, ameushauri Mkoa wa Shinyanga kuunda kamati ya kuchunguza ujenzi wa mradi wa machinjio ya mifugo ya kisasa iliyopo Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, ambayo imetumia Sh. bilioni 5.1, lakini haijakamilika, huku akisema imejengwa chini ya kiwango.

Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, na Ajira), alibainisha hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua machinjio hiyo, na kubainisha kutoridhishwa na ujenzi huo.

Alisema Sh. bilioni 5.1 ambazo zimetumika kujenga machinjio hiyo ingekuwa kwenye hatua nzuri ya ukamilishaji, lakini mpaka sasa hakuna dalili zozote za kukamilika, huku ikiwa bado ina upungufu mwingi.

"Kwa nafasi yangu ya ubunge, sikubaliani na hadhi ya machinjio hii, ina upungufu mwingi sana ukilinganisha na gharama ya fedha ambazo zimetumika kwenye ujenzi, ipo chini ya kiwango," alisema Katambi.

"Kwa nafasi yangu ya Naibu Waziri kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ninaye shughulika na Kazi, Vijana, na Ajira, hili suala nalichukua na kwenda nalo pia kwa wizara husika, haiwezekani Shinyanga tuendelee kuwa na historia ya viwanda kushindwa kukamilika kikiwamo kile cha nyama Old Shinyanga," aliongeza.

Alisema machinjio hiyo itakapokamilika itatoa ajira nyingi kwa vijana, kukuza uchumi wa wafugaji na mkoa wa ujumla, na kuufanya Mji wa Shinyanga kuwa na mzunguko wa fedha tofauti na ulivyo hivi sasa.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, alisema mradi ulianza kujengwa rasmi mwaka 2018 kwa gharama ya Sh. bilioni 5.57, na fedha zote zilishatolewa kwa mkandarasi, na ulikuwa ukamilike mwaka 2019, lakini mpaka sasa unasuasua.

Alisema serikali imeshasaini tena kiasi kingine cha Sh. milioni 171, kwa ajili ya kukamilisha upungufu uliyopo, ili ukamilike na kuanza kufanya kazi, huku akitoa wito kwa wataalamu wa serikali waisimamie vyema miradi ya maendeleo ya wananchi ijengwe kwa kiwango na wakati.

HABARI KITAIFA

## ‘Sifa za mabalozi wa Tanzania hizi’

Na Maulid Mmbaga

MDAU wa maendeleo, Dk. Salma Ahmed, ameeleza mtazamo wake juu ya suala la uteuzi wa mabalozi watakaoiwakilisha Tanzania katika mataifa mbalimbali duniani, ambao unaotarajiwa kufanyika siku za karibuni.

Dk. Salma, ambaye ana shahada ya Uzamivu (PhD) kutoka Chuo Kikuu cha Monash nchini Australia, pia amefanya kazi katika taasisi ya jinsia. Aidha, ana machapisho kadhaa pamoja na majarida katika maendeleo ya dunia, ikiwamo jarida la mafunzo ya maendeleo, sayansi ya Biosocial na utafiti wa Demografia.

Rais Samia Suluhu Hassan tangu ashike nafasi hiyo alianza na teuzi katika wizara mbalimbali pamoja na makatibu wakuu na wakuu wa taasisi za serikali, huku jana akidokeza kwamba anajipanga kuwateua wakuu wa mkoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

Mdau huyo aliyasema hayo kupitia taarifa aliyoitoa jana ambapo alieleza kuwa katika kipindi hichi ambacho Rais Samia anatarajia kufanya uteuzi wa mabalozi na kufanya marekebisho kwa ajili ya uchumi wa nchi, si vibaya kuiga baadhi ya nchi zilizofanya diplomasia ya uchumi wa kweli ikiwamo India, Marekani na China, ambazo zinatumia raia wao ambao ni wataalamu wanaoishi kwenye nchi husika.

Alitolea mfano balozi ya China ambayo huwatumia raia wake waliopo kwenye nchi husika kushauri juu ya biashara na uwekezaji na kigezo kikubwa wanachokitumia ni ufahamu wa lugha ya nchi, utamaduni na desturi za nchi husika.

“Kumpa ubalozi mtu asiyekuwa na ufahamu wa lugha, utamaduni na desturi ya nchi husika itaisababishia nchi kupoteza rasilimali fedha kwa sababu hataweza kufanya kazi kwa ufasaha, maana atahitaji sio chini ya miaka miwili kujua lugha na tamaduni za eneo husika.

“Itakuwa vyema endapo watachukuliwa watanzania wenye vigezo ambao wapo nchi husika ili kupunguza gharama za kuleta mtu toka wizarani, ambaye atakuja kusimamia elimu wakati hajui mfumo wa nchi hiyo au aje kusimamia kitengo cha biashara wakati hawezi kuwasiliana na wawekezaji wakubwa kwa lugha yao badala yake atapata watu wa kati na mawasiliano ya moja kwa moja yatakuwa hayapo,” alisema.

Aliongeza kuwa Tanzania bado ni taifa linalohitaji kuendelea kukua kiuchumi, hivyo ni vizuri kutumia rasilimali watu wenye vigezo wanaoishi nje ya nchi kuwakilisha katika balozi kwani itasaidia kuokoa fedha.

Aidha, alisema mwelekeo wa Serikali ya Rais Samia anadhamiria kufanya mabadiliko ya kiuchumi, hivyo alitoa wito kwa viongozi, wafanyabiashara na watanzania kwa ujumla kumuunga mkono Rais ili kuiwezesha nchi kuwa na diplomasia ya uchumi wa kweli na biashara.

# Wakazi Masasi wahofia nyumba kubomoka

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

BAADHI ya wakazi wa Mtaa wa Matankini Shuleni, Kata ya Nyasa Halmashauri ya Mji wa Masasi mkoani Mtwara, wanalazimika kukesha nje ya nyumba zao na familia zao kutokana na kuingiwa na hofu ya kubomoka nyumba zao kunakosababishwa na maji yanayopita kwenye mifereji ambayo ujenzi wake unadaiwa kujengwa holela na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Waliyasema hayo kwa nyakati tofauti walipokuwa wakizungumza na gazeti hili kuhusu athari walizozipata kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha wilayani hapa takribani kila siku.

Walisema kufuatia mvua kubwa zinazoendelea kunyesha hivi sasa huwenda mvua hizo zikasababisha athari kubwa ya kubomoka kwa nyumba za wakazi wa mtaa huo na sababu pekee ya athari hizo ni mifereji ya maji ambayo imejengwa vibaya na TARURA Halmashauri ya mji Masasi ambayo imekuwa ikimoboka na mmomonyoko wake unafika kwenye kuta za msingi za nymba za wananchi.

Amina Nachungulu, mkazi wa Matankini, alisema viwanja hivyo walipimiwa na idara ya ardhi ya halmashauri hiyo na kupewa ofa na kulipa gharama zote stahiki, ila wanashangazwa kuona viwanja hivyo kuwapo katika mifereji ya maji.

Alisema kufuatia nyumba hizo kuwa katika hatari ya kubomoka baada ya mifereji ya maji kubomoka kila siku na mmomonyoko wake kuelekea kwenye makazi ya watu, jambo linalosababisha hofu kwa wakazi hao.

Naye Abiba Pangomwa, mkazi wa mtaa huo, alisema nyumba yake ipo hatarini kubomoka wakati wowote kwa sababu tayari mmomonyoko wa mifereji umeshafika karibu na nyumba yake, hivyo anaomba serikali kuchukua hatua mapema kabla ya athari kutokea.

Amisi Abdallah, alisema lawama zao wanazipeleka kwa TARURA Halmashauri ya Mji Masasi kwa kumwaga kifusi cha mchanga ovyo na kufanya ujenzi usiozingatia viwango.

Naye mwenyekiti wa serikali ya mtaa huo, Hamisi Namtole, alisema suala hilo walishalifikisha katika uongozi wa juu wa serikali, na kwamba hata yeye ameingiwa na hofu ya baadhi nyumba hizo huenda zikabomoka.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Mtwara, Wilson Mwita, alipoulizwa kuhusu hali hiyo, alisema wanalitambua na kwamba watafika katika mtaa huo kwa ajili ya kutafuta suluhisho.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, alisema alishatuma timu maalumu ya kwenda katika eneo hilo kuona namna ya ujenzi bora wa mifereji.



Ofisa Muuguzi Msaidizi wa Kituo cha Afya Pasua, Mwantumu Silayo (katikati), akizungumza na maofisa wa Benki ya NMB, waliotembelea kituo hicho, wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki, kuangalia jinsi vifaa tiba vilivyotolewa na benki hiyo mwaka 2020 vinavyosaidia kuboresha huduma za afya kwa wakazi wa Kata ya Bomambuzi. Kushoto ni Meneja wa NMB tawi la Nelson Mandela, Praygod Godwin na Ofisa Uwajibikaji kwa Jamii wa benki hiyo, Aloyce Kikois. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Kikwazo cha utunzaji, usimamizi misitu hiki

**Na Said Hamdani,** LINDI.

UONGOZI wa Kijiji cha Mchichili, Wilaya ya Ruangwa, Mkoa wa Lindi, umetaja kinachodaiwa kukwamisha usimamizi na utunzaji wa misitu ni wafugaji na wakulima kuvamia maeneo ya hifadhi kufanya shughuli zao za kibinadamu.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Husna Kijazi, aliyaeleza hayo alipozungumza na waandishi wa habari walitembelea kijijini hapo kuona shughuli za kimaendeleo zinazofanywa na jamii.

Kijazi alisema vikwazo vingine vinavyoikabili hifadhi za misitu iliyopo katika maeneo ya kijiji hicho, ni uvamizi wa mifugo unaofanywa na wafugaji, wakulima na uvunaji haramu wa mazao yanayotokana na misitu na kukosekana kwa soko la uhakika kwa jamii ya miti isiyofahamika.Kijazi alisema iwapo serikali itakipa kijiji hicho kipaumbele cha kuvuna, kununua na kuuza mazao yanayotokana na misitu iliyopo kwenye hifadhi ya vijiji kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, kutasaidia kukuza soko la ndani na kupunguza tatizo hilo kwa jamii.Pia, alishauri kamati za mali asili kupewa mafunzo ya mgambo ili kusaidia uvamizi wa uvunaji haramu wa rasilimali misitu na wafugaji kuendelea kuvamia bila kufuata taratibu zilizopo kutoka mamlaka husika.

Alisema kwamba licha ya uwapo vikwazo hivyo, yapo baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu ya hifadhi za vijiji, ukiwemo ujenzi wa ofisi za serikali za vijiji, zahanati, nyumba za kuishi walimu, vyumba vya madarasa, maabara, vyoo, utengenezaji wa madawati na ununuzi wa trekta la kijiji.

# Kigezo kupanga shule kwa ubora chatajwa

SERIKALI imetaja kigezo kinachotumika kuzipanga shule kwa ubora wa ufaulu kwenye halmashauri na mikoa katika mitihani ya kitaifa.

Miongoni mwa kigezo ni wastani wa alama kwa Shule za Msingi na ufaulu wa watahiniwa kimadaraja na kimasomo kwa shule za sekondari.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni vigezo gani hutumika kushindanisha ufaulu kwa shule za msingi na sekondari kwa halmashauri na mikoa hapa nchini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga, alisema mpangilio wa ubora wa ufaulu kwa halmashauri na mikoa hutegemea wastani wa ufaulu wa shule zilizopo katika maeneo husika.

"Shule za msingi hupangwa katika mpangilio wa ubora wa ufaulu kwa kuzingatia kigezo cha wastani wa alama walizozipata watahiniwa wote wa shule husika katika masomo yote waliyoyafanya,"alisema.

Aidha, alisema wastani huo hupatikana kwa kufuata hatua mbalimbali ikiwamo kukokotoa jumla ya alama walizopata watahiniwa wote wa shule husika kwenye masomo yote waliyoyafanya.

"Kukokotoa wastani wa alama wa Shule kwa kugawanya jumla ya alama walizopata watahiniwa wote wa shule kwa idadi ya watahiniwa wa shule husika," alisema.

Kwa upande wa shule za sekondari, alisema mpangilio wa ubora wa ufaulu huzingatia kigezo cha wastani wa ufaulu wa watahiniwa kimadaraja na kimasomo.

"Wastani huo hupatikana kwa kukokotoa wastani wa ufaulu wa watahiniwa wa shule husika kimadaraja na kimasomo, jumla ya wastani huo wa ufaulu wa shule wa kimasomo na kimadaraja hukokotolewa tena ili kupata ubora wa ufaulu kwa kila shule," alisema.



Baadhi ya wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakiingia bungeni kwa ajili ya kikao cha nne, mkutano wa tatu wa Bunge la 12, linaloendelea jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Tanzania ina wafungwa, mahabusi 33,473

BUNGE limeelezwa kuwa hadi kufikia Machi 30, mwaka huu idadi ya wafungwa na mahabusi nchini ni 33,473.

Kati ya hao waliohukumiwa ni 16,735 na mahabusi ni 16,738 huku uwezo wa magereza nchini ni kuhifadhi wafungwa na mahabusi 29,902.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Konde (ACT-Wazalendo), Khatib Said Haji.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali inachukua hatua gani ya dharura kukabiliana na hali ya mrundikano mkubwa wa mahabusi katika magereza.

Akijibu swali hilo, Chilo alisema serikali inatambua uwapo wa kero ya msongamano wa wafungwa na mahabusi magerezani na imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na hali hiyo.

Hata hivyo, alisema katika kukabiliana na kutatua kero ya msongamano wa mahabusi nchini serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali zikiwamo ushirikishwaji wa vyombo vya haki jinai.

Pia alisema kufanya mabadiliko ya Sheria ya mwenendo wa makosa ya Jinai ya Mwaka 2009, Ushirikishwaji wa Mahakama na Jeshi la Magereza katika kutumia mfumo wa Tehama (Video Conference).

"Kufanya upanuzi na kujenga magereza mapya ya wilaya ambazo hazikuwa na Magereza (Mfano Ruangwa, Chato), utoaji wa dhamana kwa masharti nafuu, kuanzishwa kwa mahakama zinazotembea (Mobile Court) kwa mashauri madogo madogo yanayotolewa uamuzi pasipo watuhumiwa kupelekwa magerezani na kutoa elimu kwa raia kutojihusisha na vitendo vya kihalifu," alisema.

# Mbunge ataka ujenzi wa lami Kilindi-Gairo

MBUNGE wa Kilindi (CCM), Omari Kigua, ameitaka serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kilindi hadi Gairo kwa kuwa ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Morogoro na Tanga.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alihoji lini serikali itaanza kutekeleza ahadi ya muda mrefu ya ujenzi wa barabara hiyo.

"Barabara ni uchumi na ndio kila kitu, swali hili naliuliza kwa mara ya pili lakini majibu ni yale yale, kwa kuwa barabara hii kipindi cha mvua haipitiki, ni barabara yenye uchumi wa hali ya juu sana, hii barabara ni ahadi tangu Rais mstaafu Jakaya Kikwete,"alisema.

Alihoji wananchi watarajie lini barabara hiyo kujengwa.

"Je, Naibu Waziri yupo tayari kutuma timu yake kwenda kukagua kuona hali halisi maana barabara haipitiki na wananchi wanapata adha kubwa?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema barabara ya Kilindi – Iyogwe – Gairo yenye jumla ya kilometa 115.7 ni barabara ya mkoa inayounganisha mikoa ya Tanga na Morogoro kupitia wilaya za Kilindi na Gairo na inahudumiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) katika mikoa ya Tanga na Morogoro.

Aidha, alisema kutokana na ufinyu wa bajeti, kwa sasa serikali haijapata fedha za kuanza ujenzi wa barabara ya Kilindi – Iyongwe – Ngilori – Gairo kwa kiwango cha lami.

"Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii ili kuhakikisha kuwa inaendelea kupitika vizuri majira yote ya mwaka," alisema.

Kasekenya alisema barabara zote ni muhimu kwenye masuala ya uchumi na kwamba katika Ilani ya Uchaguzi ya miaka mitano zitajengwa kwa kipindi hicho kulingana na upatikanaji wa fedha.

"Kuhusu madaraja matatu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wiki hii Meneja Tanroads wa Tanga na Morogoro watatembelea hizi barabara na kuona kero za madaraja ili kutokatisha usafiri wa mikoa hii," alisema.








Ukurasa 14

**Siku 19 za Rais Samia zatengua msimamo wa Lipumba kususa**



Ukurasa 12

**MWANZO UHURU WA MSUMBIJI NCHINI**

siasa

JUMATANO APRILI 7, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

MZEE MASALAKULANGWA;

# Nguzo ya CCM Kanda ya Ziwa amkubali Rais akimpa 'tano'

• Apima darubini yake, neema yaja

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

SIKU zinazidi kuhesabika, Rais Samia Suluhu Hassan, yuko madarakani akiwa na mambo kadhaa aliyoyafanyia uamuzi, hali kadhalika hotuba zake kueleza msimamo aliyonayo, kuhusu kile Tanzania inapaswa ifanyiwe.

Pia, katika hilo ni jana tu alitoa hotuba ndefu kwa umma wa Watanzania, baada ya kuaapisha viongozi waandamizi wa kiserikali walioteuliwa kwa nafasi mbalimbali.

Sambamba na hili, amewaanikia viongozi kwamba hali ya kupanga vyema safu ya utendaji katika maeneo ya kimkoa, bado anaendelea katika maeneo mengine muhimu kwa utendaji.

Hapo alianika namna anavyotaka serikali yake itumike katika kila sekta, pia wizara zake, akiainisha kila moja anavyohitaji iwe.

Ili kupata tathmini ya awali , Nipashe iligonga hodi nyumbani kwa mwanasiasa mwandamizi na sehemu ya wazee wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mwanza, pia mdau kitaifa, Mzee Charles Masalakulangwa.

Anaanza kumtambulisha kwamba, Rais Samia amewaonyesha Watanzania uwezo mkubwa wa kuliongoza Taifa katika kile mzee huyo amekiita 'umakini bila kutokuyumba.'

Gwiji huyo wa siasa, anatafsiri haiba ya Rais kuwa na mpole, lakini ana kauli zilizojaa busara, msimamo na anachokiita "uangalifu mwingi wa kutosha kusimamia nchi," hali inayowapa matumaini makubwa ya kuwavusha kimaendeleo.

Hapo, mkongwe huyo anaingiza ushauri wake kumtaka mkuu wa nchi kuendeleza uimara wake na kutosita kuwachukulia hatua watendaji watakaotaka kumwangusha katika kuchapa kazi, wakiwamo wanaokiuka nidhamu na maadili ya utumishi wa umma.

"Rais Samia anatakiwa kuwa mkali, hasa kwa mawaziri wapya aliowateua na aliowabadilisha wizara, anapoona wanakwenda tofauti na serikali yake." anasema Mzee Masalakulangwa.

**KAZI KWA BIDII**

Pia, anakumbusha kuwapo waliozoea kufanya kazi kwa kusimamiwa na kusukumwa ndipo ionekane bidii, anawataka kubadiika ili kumsaidia Rais kuchapa kazi, badala ya kuwachelewesha wananchi na taifa kufikia malengo yenye mafaniko ya kiuchumi.

Anaeleza imani yake kwamba, kiongozi huyo wa sasa yuko sambamba na kasi ya utendaji za mtangulizi wake, akimpa wasifu wa ujasiri, weledi na uzoefu wa kutosha, tafsiri walionayo ya matumaini Watanzania wanayo kwake.

Mzee Masalakulangwa, anataja umuhimu katika usimamizi wa miradi kama afya, maji, kilimo, ujenzi wa stendi za mabasi mikoani na masoko makuu yasiyokamilika.

"Mambo matatu anayotakiwa kuyakamilisha, kuyatekeleza ni miradi mikubwa ambayo ni ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere, reli ya kisasa(SGR) pamoja na ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi," anasisitiza Mzee Masalakulangwa.

Anabainisha kuwa, endapo atavuka mtihani wa kuikamilisha miradi iliyoachwa na mtangulizi wake, itakuwa mrejesho wa matumaini makubwa zaidi kwa Watanzania, kuendelea kumwamini na kuleta mabadiliko kiuchumi.



Mzee Charles Masalakulangwa. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

Pia mwanasiasa huyo anatoa angalizo kwa serikali na chama tawala CCM, kuwa makini na aina yoyote ya dhana ya makundi, kwani kuwa nayo ni ushindi

**UCHUMI NA KODI**

Pia Masalakulangwa anafafanua kwamba, serikali inatakiwa kutilia mkazo suala la kilimo, ufufuaji na ujenzi wa viwanda, ili kukuza uchumi wa nchi, kwa sababu uzalishaji mkubwa wa malighafi unatokana na sekta ya kilimo.

Aidha sekta ya kilimo ndiyo yenye ajira kubwa kwa wananchi wa kawaida, ikikadiriwa kuwa asilimia 80 ya Watanzania hufanya shughuli za kilimo, biashara na ufugaji.

Mzee Masalakulangwa anasema, lakini licha kilimo kuwa pacha wa viwanda, bado serikali inakabiliwa na ugumu wa kushindwa kufikia malengo mazuri ya kujenga viwanda au kufufua vya zamani ambavyo vilikufa tangu enzi za utawala wa awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Nyerere.

Akitoa mfano wa kiwanda kilichopo jijini Mwanza cha kutengeneza nguo maarufu Mwatex, ambacho kilifufuliwa na mwekezaji na kuanza kuzalisha nguo, anakiri haijafikia rekodi ya zama hizo.

Kwa mujibu wa mwanasiasa huyo, mwenyeji wa Mwanza, Mwatex ya wakati huo ilishaweka historia ya kuajiri zaidi ya wafanyakazi 4,000, mbali na idadi kubwa ya wajasiriamali jirani kama vile Mamalishe na Babalishe, waliopata fursa kuwauzia wafanyakazi chakula, nje ya kiwanda.

INAENDELEA UK.14

# MWANZO UHURU WA MSUMBIJI NCHINI

• Faragha Nyerere, FRELIMO 1962 Dar, 1968 kwao 'wakaanzisha'; 1969 Mondlane kauawa
• Makazi ya kudumu Samora alikojipanga • Pajue Rais Nyusi alikoanza shule, Tunduru

**Na mwandishi Wetu,** aliyekuwa ziarani Tunduru



Kamanda wa wanaharakati wa FRELIMO, Samora Machel, alipokuwa na wapiganaji wake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

NCHI ya Tanzania wakati huo ikiwa chini ya uongozi wa Rais Julius Nyerere, ilishiriki kikamilifu kwenye harakati za ukombozi kusini mwa Afrika.

Msumbiji, kikoloni la Wareno ni miongoni mwa nchi ambazo hazitaisahau Tanzania ilivyotoa mchango wake hadi kusababisha nchi hiyo kupata uhuru wake toka kwa wareno mwaka 1975.

Kwa waliokuwapo zama hizo, siku ya uhuru wa Msumbiji mwaka 1975, wana kumbukumbu ya sherehe kubwa, raia wa nchi hiyo walivyofurahia, kila aina ya kusherekea kulitawala, pasipo kusahau ngoma maarufu wakati huo la kabila la kimakonde 'sindimba.'

Miji ya Kusini mwa Tanzania, kukiwamo Nachingwea na Liwale, kulijaa wenyeji wakazi, raia wa Msumbiji, huku jijini Dar es Salaam, hasa maeneo kama Msasani, Kinondoni na Bunju, pia mitaa ya Zanzibar, mathalan kuelekea Uwanja wa Ndege walipatikana kwa wingi.

### SIMULIZI RASMI

Alfonso Kaidavid ni Mhifadhi kwenye Makumbusho ya Taifa ya Msumbiji yaliyopo Matchedje, katika Jimbo la Niassa, anasimulizi namna serikali ya Msumbiji, iliamua kuanzisha Makumbusho katika eneo hilo, kutokana na kufanyika Mkutano wa Pili mwaka 1968, uliosababisha nchi hiyo kupata uhuru wake.

Anasema Mkutano wa Kwanza wa harakati za kuikomboa Msumbiji, ulifanyika jijini Dar es Salaam mwaka 1962, katika ukumbi wa Arnatoglu, eneo la Mnazi Mmoja, ukiwa ni mwaka mmoja, tangu uhuru wa Tanganyika.

Kwa mujibu wa Mhifadhi Kaidavid, mkutano huo uliongozwa na Rais Julius Nyerere, aliyekutana wa Tanganyika wakati huo, upande wa Msumbiji, walikuwapo viongozi waandamizi wa chama cha FRELIMO, wakiwamo kiongozi mkuu Dk. Eduardo Mondlane na Samora Machel, kamanda wa wapiganaji wao.

Mhifadhi Dk. Kaidavid anasema, mkutano wa pili ulifanyika kwa siku tano katika eneo la Matchedje, kuanzia Julai 20 hadi 25, mwaka 1968 na uliongozwa na viongozi waandamizi walikuwapo katika mkutano wa kwanza, jijini Dar es Salaam.

"Makumbusho haya tumeanzisha ili Wana - Msumbiji, Watanzania na wageni wengine kutoka nchi mbalimbali, waweze kujua ni namna gani nchi ya Msumbiji ilipambana katika kuikomboa nchi toka kwa wakoloni wareno ambao waliutawala kwa miaka mingi," anasimulia Kaidavidi.

Anarejea nyendo zao kwamba viongozi wa FRELIMO Dk. Edward Mondlane kwa kushirikiana na Samora Machel, ambao wameshafariki, walipata mafunzo mbalimbali nje ya Msumbiji, kuhusu stadi na mbinu za kumng'oa mkoloni.

### MBINU ZAO

Mhifadhi huyo anasema kabla ya kuamua kumwaga damu viongozi hao walijaribu kuzungumza na wareno ili wakubali kwa hiyari kutoa uhuru wa Msumbiji, hata hivyo ilishindikana ndipo waliamua kutumia njia ya bunduki.

> Samora alifariki kwa ajali ya ndege, ikidaiwa ni hujuma za kisiasa, mnamo Oktoba mwaka 1986, alishatumikia urais wa nchi yake kwa miaka 11.



Mkuu wa FRELIMO, Dk. Eduardo Mondlane, alipokuwa na Kamanda wake Mkuu, Samora Machel.

Historia inaonyesha Wareno walifika nchini Msumbiji mwaka 1498, walipokuwa katika safari ya kwenda nchini India, hata hivyo waliamua kubaki Msumbiji, baada ya kubaini kuwapo utajiri mkubwa wa madini na meno ya tembo.

Akizungumzia vivutio vya utalii vilivyopo eneo hilo la kihistoria la Matchedje, Kaidavid anasema hadi sasa yamebakia masalia ya vibanda, ambavyo viongozi wa kitaifa waliishi kwa siku tano kufanya mkutano wa pili mwaka 1968, ambao ndio mzizi wa uhuru wa Msumbiji.

Kivutio kwenye eneo hilo ni kuwapo 'gogo' mwaka 1968 waliokalia Rais Julius Nyerere wa Tanzania, Rais Edward Mondlane wa Msumbiji na Mkuu wa Majeshi, alikuwa Samora Machel waliokaa kwenye gogo hilo kwa siku tano, wakijadili namna ya kuikomboa Msumbiji kutoka utawala wa wareno.

"Viongozi hao mwaka 1968 walijadili wakiwa wamekaa kwenye gogo hili ambalo hadi leo bado lipo likiwa vile vile bila kuoza, tumelihifadhi kama kumbukumbu muhimu kwenye harakati za ukombozi wa nchi ya Msumbiji," anasisitiza mhifadhi huyo.

Maeneo mengine ambayo ni kivutio kwenye eneo hilo ni kuwapo kibanda alicholala kwa siku tano Rais kiongozi mkuu wa chama FRELIMO, Dk. Eduardo Mondlane mwaka 1968.

Hata hivyo, hakudumu maishani, kwa sababu alifariki mwaka mmoja baadaye, mnamo Februari mwaka 1969, nchini Tanzania kupitia bomu aliyotegeshewa, ikidhaniwa ni barua kwake.

Mahali hapo, Matchedje, katika jimbo la Nassa, Msumbiji pana kibanda alichokuwa akilala Mkuu wa Majeshi wa FRELIMO wakati huo, Samora Machel kwa siku tano na kibanda kingine kilitumiwa na wana habari kwa siku hizo alizokuwapo kiongozi huyo wa ulinzi.

Samora naye alifariki kwa ajali ya ndege, ikidaiwa ni hujuma za kisiasa, mnamo Oktoba mwaka 1986, alishatumikia urais wa nchi yake kwa miaka 11.

### KAMBI TUNDURU

Pia nchini Tanzania, kuna eneo la Masonya, ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, ambako kuna utajiri wa malikale na utambulisho wa Taifa, ingawa huenda bado halifahamika na wengi.

Ni mahali penye ukubwa wa ekari 100, likiwa na vivutio adimu vya utalii wa malikale, zikiwamo nyumba yenye utambulisho 'Namba A 10' iliyokuwa inafikiwa na kuishi Marais Nyerere na Samora wa Msumbiji, kuanzia 1966, ndani ya harakati za ukombozi za Msumbiji.

Mhifadhi wa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Bartazar Nyamusya, anasema viongozi hao pia wakiwa katika nyumba hiyo, walitumia jengo dogo maalum lililopo jirani ya nyumba hiyo, kama chumba cha mawasiliano yote na nchi zilizokuwa katika harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika.

Kati ya nyumba ya viongozi hao hadi iliko jengo dogo la mawasiliano, kulijengwa handaki lililopo hadi sasa, lililotumiwa na viongozi hao wa Tanzania na Msumbiji.

Eneo la malikale la Masonya lenye ukubwa wa ekari 100 lipo umbali wa kilometa 12 Kaskazini mwa mji wa Tunduru, bado halijaendelezwa sana.

Historia inaonyesha kuwa, Rais wa sasa wa Msumbiji Filipe Nyusi, alisoma katika Shule ya Msingi Frelimo, iliyokuwapo katika eneo la Masonya na walifika hapo na wazazi wao wakaishi mwaka 1970, alipokuwa na umri wa miaka 11.

Serikali kwa sasa inalitumia eneo la malikale la Masonya, kwa shughuli za kielimu, ambako kumejengwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Masonya.

Kabla ya mwaka 1966, eneo la malikale la Masonya ilikuwa msitu, hadi mwaka huo, serikali iliwapokea watu kutoka nchini Msumbiji na kuwakabidhi eneo hilo katika kipindi chote cha kupigania uhuru nchini Msumbiji.

Nurdin Seleman, Mwenyekiti wa Kijiji cha Masonya, anasema palikuwa ni kambi ya wapigania uhuru wa nchi ya Msumbiji na eneo hilo lina malikale zilizokuwa zinatumiwa na wananchi wa Msumbiji.

Anasema, ni mahali linatembelewa mara kwa mara na wananchi wa Msumbiji, akiwamo Balozi wao na serikali ya kijiji hicho inaendelea kuzitunza malikale ambazo ni muhimu kwa vizazi vya sasa na vijavyo kwa maendeleo ya nchi zote mbili.

Erick Soko, ni Ofisa Elimu Msaidizi wa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji, anayesema tangu mwaka 1966 walipokabidhiwa eneo hilo la Masonya, raia wa Msumbiji wamekuwa wakifanya ziara kuzuru eneo waliloishi viongozi mashuhuri wa nchi hiyo, akiwemo Hayati Rais Samora Machel.

"Katika kipindi cha miaka 10 kuanzia 1966, wanawake kutoka nchini Msumbiji wamekuwa wanaishi katika eneo la Masonya," anaeleza Soko na kuendelea: "Umoja wa Wanawake wa Msumbiji unaojulikana kwa OMM ulianzia Masonya mwaka 1973."

Anasimulia ilipofika mwaka 1975 baada ya uhuru wa Msumbiji, ndipo kambi ya Masonya ilivunjwa rasmi na wana Msumbiji walirejea katika nchi yao na hadi mwaka 1989 eneo hili lilibaki bila matumizi.

### SERIKALI TUNDURU

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, anazitaja rasilimali adimu zilizopo katika eneo la malikale la Masonya, kuwa ni majengo 13 ya FRELIMO na masalia ya kale ya nyumba za viongozi wa kitaifa, Mwalimu Julius Nyerere na Samora Machel.

Mtatiro anasema licha ya eneo hilo kuwa na majengo mengi yaliojengwa na watu wa Msumbiji na mengine ya serikali, bado kuna magofu na majengo mengi chakavu, hivyo ni muhimu eneo hilo kuboreshwa na kuhifadhiwa kwa malengo endelevu.

> Niliagiza halmashauri zote nchini kutunza maeneo yote ya kihistoria. Mimi nitatembelea kila halmashauri nchi nzima, kuhakikisha maeneo yenye utajiri wa kihistoria yanatunzwa na kuhifadhiwa.

Kutokana na umuhimu wa eneo la Masonya katika harakati za ukombozi kusini mwa Afrika, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Innocent Bashungwa, ametembelea eneo hilo na kuagiza maeneo yote ya kihistoria yalindwe na kutunzwa kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho.

Waziri Bashungwa analitaja eneo la Masonya kuwa limesheheni utajiri mkubwa wa historia ya Tanzania na namna taifa ilivyoshiriki katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Pia anaeleza kufurahishwa na nyumba uwapo wa nyumba iliyotumiwa na Rais wa zamani wa Msumbiji, Samora Machel kati ya mwaka 1966 hadi nchi ilipopata uhuru mwaka 1975, pia makazi kama hayo ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere.

"Historia yote tajiri imezama katika Kata ya Masonya. Niliagiza halmashauri zote nchini kutunza maeneo yote ya kihistoria. Mimi nitatembelea kila halmashauri nchi nzima, kuhakikisha maeneo yenye utajiri wa kihistoria yanatunzwa na kuhifadhiwa," anasisitiza.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Tunduru, Mwajuma Abasi Nasombe, anautaja urithi mwingine kwenye eneo la Masonya, ni ukumbi wa semina aliyokuwa anatumia Samora Machel kutoa mafunzo mbalimbali na majengo 11 ambayo kwa sasa ni madarasa ya wanafunzi wa sekondari ya wasichana Masonya.

Anasema kuanzia mwaka 1990, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, ilianzisha Shule ya Sekondari ya Wasichana Masonya na hadi kufikia mwaka 2014, inachukua wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita.




Majengo ya makazi alikoweka kambi Samora Machel na wapiganaji wenzake wa Msumbiji, kuhusu Uhuru wa Msumbiji, eneo la Masonya, wilayani Tunduru. Ndiko alikoanzia shule Rais Filipe Nyusi miaka 51 iliyopita **PICHA ZOTE: MAKTABA**




Makumbusho ya Matchedje nchini Msumbiji, ambako mkutano wa pili kuhusu Uhuru wa Msumbiji uliofanyika chini ya Rais Julius Nyerere na kuwezesha harakati za ukombozi nchini humo.

JUKWAA LA UONGOZI

# Siku 19 za Rais Samia zatengua msimamo wa Lipumba kususa

• Kijo – Bisimba: Mwacheni, Katiba haimfai sasa

**Na Sabato Kasika**

HADI sasa ni chini ya mwezi mmoja, tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, kutimiza mchakato wa kikatiba, kuziba pengo la kifo cha Rais John Magufuli.

Iko bayana vyama vingi vya kisiasa ambavyo ndani ya utamaduni wa kisiasa, ni wapinzani wa watawala Chama Cha Mapinduzi (CCM), vimejitokeza hadharani kumpa pongezi 'kumkubali'.

Ndani ya pongezi hizo kwa vyama washindani wa siasa, wengi wamekuwa na lugha inayofana ikiwa na 'bando' la kufufua hoja ya Katiba Mpya, ambayo Hayati Rais DK. John Magufuli, aliweka wazi kwamba haikuwa kipaumbele cha mkakati wake.

Dai lao linajikita katika wanachokiita hatua ya rasimu ya pili wanayodaiwa viliondolewa vifungu muhimu na Bunge Maalum la Katiba, ambalo kuna vyama vya upinzani vilisusia.

Kwa ujumla simulizi za Bunge hilo la Katiba na maudhui ya kilichojiri kikaoni huko mjini Dodoma, Rais Samia si geni kwake kwani alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba, la mwaka 2014.

Kama wazungu walivyo na tamathali yao 'kutoka mdomoni mwa farasi' kwa maana ya mhusika halisi ndiye anapaswa kutamka jambo, Nipashe jana ilimtafuta Mwenyekiti wa Chama Cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, aweze kunena lake kuhusiana na hilo.

Itakumbukwa, Prof. Lipumba akiwa mshiriki wa kila mwaka wa uchaguzi mkuu kuwania nafasi ya urais tangu mwaka 1995, mwaka jana aligeuka kwa kutamka chama chake kisingeshiriki tena katika uchaguzi.

Alitaja sababu za kutoridhika ni kilio katika mfumo wa uchaguzi na walakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Hata hivyo, ujio wa Rais Samia, umemuunda Prof, Lipumba mpya na chama chake cha CUF, akionyesha imani kwamba Rais Samia anaweza kuiletea nchi katiba mpya, kwa madai ana uzoefu na mambo ya katiba na si mtu wa kukurupuka.



Profesa Ibrahim Lipumba. **PICHA: MTANDAO**

> Pia, Rais Samia alionya watendaji kuacha kampeni kwa ajili ya uchaguzi mkuu.

Prof. Lipumba anasema: "Kwanza kabisa Rais Samia ni mpole, mtulivu, msikivu, anafikiri kabla ya kutenda na uzoefu kwa mambo ya katiba, kwani alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba."

Kiongozi huyo wa CUF na mwanazuoni wa zamani wa uchumi, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anaiambia Nipashe kuwa katiba iliyopo haiendani na mabadiliko ya sasa, hasa kuwapo kwa vyama vingi nchini na Tume ya Taifa ya uchaguzi, bado ni ileile, akidai haiko huru.

"Sisi kama chama, bado tuna matumaini na Rais Samia, pia tunamuomba aharakishe mchakato wa kuwapo kwa katiba mpya ili tuachane na hii yenye viraka," anasema.

**ILIVYOKUWA AWALI**

Prof. Lipumba, aliyewania urais katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, alitoa msimamo wa chama hicho, baada ya uchaguzi huo kuwa CUF haitoshiriki tena katika uchaguzi.

Madai yake yalikuwa kwamba, uchaguzi huo haukuwa huru na haki, akitolea mfano wa madai kwamba wagombea wa upinzani walivyoenguliwa kwa pingamizi na kuzuiliwa wakala wa upinzani kwenye vyumba vya kupigia kura.

Baada ya kutoa tangazo la kususia uchaguzi aliahidi kuanzisha mazungumzo na jumuiya za kimataifa na taasisi zinazofuatilia masuala haki na demokrasia, kuziomba kuisadia Tanzania kujenga misingi aliyoziita "za kudumu za demokrasia na utawala bora."

Hata hivyo, msimamo wake wa sasa, anaamini kuna uelekeo wa kupata tume huru na katiba mpya, kwa madai kwamba kauli za rais zinaonyesha nia njema ya kuwaunganisha Watanzania.

Rais Samia anayeendelea kuwajibika na masuala mtambuka ikiwamo kuomboleza kifo cha mtangulizi wake, kuteua viongozi na watendaji, maelekezo ya kikazi kama ilivyokuwa jana aliposhuhudia viapo vya wateule wake na hotuba za malekezo, alishaweka bayana haja ya 'subira kidogo' katika suala hilo la katiba mpya.

Mkurugenzi mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (LHRC), Dk. Helen Kijo-Bisimba, anaungana na dhana ya 'subira kidogo' akiwataka wanasiasa kumpa nafasi Rais Samia, kwanza kabla ya suala la Katiba Mpya.

"Nilivyomuelewa Rais wetu ni kwamba anahitaji kupata muda wa kutafakari kwanza kabla ya kuchukua hatua kwenye suala la Katiba Mpya. Hivyo, ni vyema wanasiasa wakamuacha kwanza atafakari," anasema Dk. Kijo-Bisimba.

Mwanasheria huyo, anasema suala la mchakato wa katiba mpya halikuwekwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya CCM inayotumikiwa sasa, hali hiyo inayomfanya ahitaji muda wa kutosha kutafakari.

"Pia, Rais Samia alionya watendaji kuacha kampeni kwa ajili ya uchaguzi mkuu. Hapa maana yake ni kwamba, anataka utendaji wao ndiyo uwauze kwa wananchi na siyo mtindo wanaotaka kuufanya," anasema.

Anafafanua kuwa serikali iliyoko madarakani ni ya CCM na watendaji wake wanatakiwa kufanya kazi za maendeleo, ili kuwafanya wananchi waendelee kukiamini chama, badala kuanza kwa vikumbo vya kusaka uongozi.

"Katika mazingira hayo hawawezi kuwatumikia wananchi, ndiyo maana Rais ameliona hilo na kulikemea na kuelekeza zaidi kwenye uchapakazi, ili kutekeleza yale yaliyomo kwenye ilani yao," anasema.

Anasema, wanapaswa kuanzisha sasa vikumbo vya kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, ni watokao vyama vya upinzani na siyo CCM, kwani inaweza kuwavuruga.

## Nguzo ya CCM Kanda ya Ziwa amkubali Rais akimpa 'tano'

**INATOKA UK.11**

Kiwanda hicho anasema kilizalisha wakati huo wa serikali ya awamu ya kwanza nguo aina ya khanga na vitenge, ambacho kwa sasa uzalishaji wake ni mdogo mno. Analalama kwamba, iwapo kutafufuliwa kwa stadi sahihi, watu wengi watawezeshwa kupata ajira mahali hapo.

Anasisitiza kwamba, katika kuinua sekta za kilimo, viwanda, biashara na mifugo kwa sababu zina umuhimu mkubwa katika ukuzaji wa uchumi wa nchi.

**MASALAKULANGWA NI NANI?**

Mzee Malasakulangwa, kitaaluma alipata elimu ya uchapishaji nchini Kenya kwa ngazi ya shahada na baadaye aliendelea na masomo hayo nchini Marekani kati ya mwaka 1977 hadi 1978.

Baada ya hapo alirejea nchini akiwa mwajiriwa wa kanisani, huku akiwa na utashi wa kisiasa na baadaye akaingia rasmi kwenye siasa, hata akashuhudiwa mwaka 1992 na baadaye ulipofika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 alikuwa mdau mkuu katika kinyang'anyiro cha makundi ndani ya CCM, kusaka mgombea urais.

Ni mara nyingine mwanasiasa huyo akaonekana tena, akiwa katika makambi ya wagombea, mwaka 2005. Ulipofika wakati wa kampeni za uchaguzi Mkuu wa 2010, Mzee Masalakulangwa aliteuliwa kuwa Mratibu wa Kampeni Kanda ya Ziwa kwa maana ya mikoa ya Kagera na Mwanza.

Anasema, kupitia wadhifa huo ndio pia ulimfungulia uenyeji wa wilayani Chato, kwa mara ya kwanza alipofika nyumbani kwa Hayati Dk. John Magufuli, kwa mara ya kwanza ikiwa ni tukio la msiba na tangu hapo kiongozi huyo alipokuwa waziri, waliendeleza uhusiano wa moja kwa moja hadi kufikia umauti wake.



# Wanufaika TASAF wajikita kilimo cha korosho

**Na Renatha Msungu, CHAMWINO**

WANUFAIKA wa Mpango wa kunusuru kaya Maskini (TASAF) wa Kijiji cha Mlowa barabarani wilayani Chamwino mkoani Dodoma, wametenga heka tano za shamba darasa kwa ajili ya kilimo cha korosho.

Walengwa hao wameamua kutenga heka hizo ambazo zitatumika kama shamba darasa kwa wakazi wa kijiji hicho na maeneo ya jirani kutokana na kilimo hicho kuwa kigeni wilayani Chamwino mkoani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea katika shamba hilo ambalo tayari limepandwa miche ya mikorosho, Mwenyekiti mstaafu wa kijiji hicho, Amosi Leuna, alisema shamba hilo litatumika kutoa elimu kwa wakazi wa maeneo hayo kutokana na wengi kutokuwa na uzoefu na kilimo cha korosho.

"Kilimo cha korosho ni kilimo cha biashara, tumejaribu zao hili na kuona linastawi, tumeona tuanzishe shamba hili ili lisaidie kuwakwamua watu kiuchumi," alisema Leuna.

Alisema kilimo hicho ni muhimu kwa wananchi kwa sababu ni zao la biashara ambalo linamwezesha mwananchi kujikwamua kiuchumi.

Alisema baadhi ya wakazi wa kijiji hicho ambao wamelima zao hilo tayari wameona manufaa yake ndio maana wameunda kikundi na kuanzisha kilimo hicho.

Naye mratibu wa zao hilo, Hosea Ndui, alisema wao kama wataalamu wataendelea kutoa elimu kwa walengwa ili kuhakikisha zao hilo linaendelea kukua katika wilaya hiyo.

Alisema, lengo lao kila mkulima wa wilaya hiyo kulima kilimo ambacho kitawainua kiuchumi hapo baadaye.

"Nawapongeza hawa walengwa wa TASAF kwa kuanzisha mradi huu wa kilimo cha korosho, ni kilimo bora cha biashara na kina manufaa makubwa," alisema Ndui.

Pia, alisema wamekuwa wakiwafuatilia wanakikundi ambao wameanzisha shamba hilo kwa ajili ya kuwapa elimu ya utunzaji wa miti ya korosho pale inapokuwa shambani.

Mmoja wa walengwa wa TASAF ambaye ni mkulima wa zao hilo, Yohana Magomba, alisema mradi wa kilimo cha korosho unahitaji maandalizi ya kutosha pamoja na uangalizi wa karibu ili uweze kupata mazao mengi kipindi cha mavuno.

Ofisa Malalamiko wa Idara ya Mawasiliano wa TASAF, Makwinja Dismas, aliwapongeza walengwa kwa kuanzisha shamba hilo kutokana na kwamba litawasaidia kuleta maendeleo katika kijijini hicho.

# YPC yataka nguvu ya vijana kutambulika kiuchumi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi inayojihusisha na masula ya vijana Tanzania (YPC), Israel Ilunde, amesema serikali na wabia wa maendeleo wanatakiwa kutambua nguvu ya vijana kwenye kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

Ilunde alisema hayo jijini Dodoma, wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kongamano la viongozi na vijana juu ya ushiriki kwenye maisha ya umma na kuimarisha mitandao (nguvu ya pamoja).

Alisema nguvu ya vijana walionayo ikitumika vyema, itasaidia kuleta mabadiliko katika uchumi kama hazina na suluhisho la kero zinazowakabili na jamii kwa ujumla.

"Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa asilimia 50 ya wakazi duniani ni vijana wenye umri usiozidi miaka 25 na kwa Tanzania asilimia 64 ya idadi ya watu wana umri chini ya miaka 24, wakati wale wenye umri wa miaka 15 hadi 35 ni asilimia 34 ya idadi ya wakazi wote.

"Hii inafanya nguvu kazi ya Taifa ambayo ni vijana kuwa asilimia 68 hivyo ni lazima vijana washiriki katika vyombo na uamuzi na michakato yote ya kidemokrasia," alisema Ilunde.

Aidha, alisema taifa lolote ambalo linapuuza au kuwasahau vijana wake lijue linafanya hivyo kwa ajili ya anguko lake siku za usoni.

Alisema kuna haja ya serikali na wadau wengine wa maendeleo kuwekeza juhudi katika kuwaandaa vijana kutimiza wajibu wao kwa wakati na kuchukua hatma za kumiliki uchumi na kutoa mchango wao kwenye uongozi wa umma na kushawishi mabadiliko ya kisera na kimaamuzi.

Hata hivyo, alisema YPC imekuwa ikiwajengea uwezo vijana kiraia na kiuchumi ili waweze kuongoza juhudi za kuendeleza jamii zao na Taifa kwa ujumla.

Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo, Irene Ringo, alisema kupitia mafunzo hayo atakuwa balozi mzuri kwa vijana kuwapa mwanga wa kuchangamkia fursa zinazojitokeza ili kupata uzoefu.

"Elimu niliyoipata nitaitumia kuwaelimisha vijana wenzangu kupenda kujitolea ili kupata uzoefu, vijana wengine tulikuwa tuwanasubiria kutafutwa na fursa au kutafutiwa, hii ni kwa sababu hatukuwa na uelewa wa mambo kadhaa kuhusu vijana ikiwamo kujitolea," alisema.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Dk. Edmund Mndolwa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, alipokuwa akimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kulia kwake ni Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Erasto Yohana Sima.. PICHA: PETER MKWAVILA

# Watoto wanaoishi mazingira magumu watoa kilio

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WATOTO wanaoishi katika mazingira hatarishi mkoani Dodoma, wameiomba serikali, mashirika, taasisi za kidini na watu binafsi kuwasaidia kupata elimu itakayowawezesha kuondokana na maisha hatarishi wanayoishi hivi sasa mitaani.

Rai hiyo ilitolewa jana na watoto hao walipokuwa wakishukuru kwa kula chakula cha pamoja na mwanachuo wa mwaka wa tatu kutoka Chuo cha Uhasibu Jijini Arusha, Emmanuel Bundala.

Mmoja wa watoto hao, Godfrey Bosco, alisema kero waliyonayo ni mtizamo hasi iliyojengeka kwa wanajaamii ya kuwaona kama watoto hao ni wa mitaani na hawawezi kupata elimu itakayowasaidia kuondokana na maisha wanayoishi hivi sasa.

"Tunawaomba wahisani mbalimbali wajitokeze kutupatia msaada wa kutusomesha, ili tuondokane na imani potofu iliyojengeka miongoni mwa wana jamii, ambao wanaotuona sisi ni machokoraa,watoto wa mitaani, wavuta ngundi na vibaka," alisema.

Watoto hao wanaoishi mitaani katika Jiji la Dodoma kutoka mkoani Kigoma, wanasema kuwa wanaishi katika mazingira hatarishi siyo kwa sababu ya wao wanapenda, bali ni matatizo ya kifamilia zao walikotoka.

Bosco alisema kuwa maisha wanayoishi ni mabaya kwani wamekuwa wakinyeshewa mvua na jua, huku wakiishi kwa kuombaomba, na wakati mwingine wakiambulia kupigwa na kufanyiwa ukatili.

"Hivyo tunaomba serikali pamoja na taasisi mbalimbali za umma na binafsi hata mtu mmoja mmoja wafanye kama alivyotukumbuka Emmanuel kwa kuja kula chakula cha pamoja na sisi ambao tunaonekana hatufai mbele ya jamii," alisema Bosco.

Kwa upande wake, Emmanuel Bundala, alisema kuwa ameshiriki na watoto hao kula chakula kwa pamoja kwa kuwa wamekuwa wakisahaulika kutokana na imani kubwa iliyojengeka kwa wanajamii kuwa wao maisha yao ni ya mitaani.

Hivyo alishauri mashirika, taasisi, serikali na watu binafsi kuwakumbuka watoto hao katika kuwapatia mahitaji mbalimbali ambayo wanayoyakosa ikiwamo elimu, afya, chakula, malazi na mavazi.

Bundala alisema kuwa watoto hao hawajapenda kuishi maisha ya mitaani bali wamejikuta hapo kutokana kila mmoja alivyolelewa kwenye familia husika.

"Nimeona taasisi na watu binafsi wakitembelea vituo vya watoto yatima na wengine katika makundi mbalimbali lakini kundi hili limesahauliwa na kutengwa,"alisema Bundala.

Makamu Katibu Mkuu Taifa, Askofu Julus Bundala kutoka Kanisa la PHAM T, aliwataka watoto hao pamoja na changamoto wanazokutananazo kuwa karibu na Mungu.

Askofu Bundala alisema watoto waishio mitaani wasijione kama ni watu wa waliokataliwa, badala yake wajione kuwa Mungu anaweza kuwabadilisha tabia zao na hatimaye wakaondokana na mateso waliyonayo.



# Mbalizi waanika sababu kumuenzi JPM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wamehitimisha siku 21 za maombolezo ya kitaifa ya msiba wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, kwa kudai kuwa watamkumbuka kwa kuwasaidia kumaliza tatizo la maji.

Wakizungumza jana na Nipashe, wananchi hao walisema kwa muda mrefu walikuwa wanapata shida ya maji kutokana na vyanzo vilivyokuwapo kutokidhi mahitaji ya mji huo.

Mmoja wa wananchi hao, Samora Mwenizumba, alisema wakati wa ziara ya Hayati Magufuli mkoani Mbeya, wakazi wa mji huo walisimamisha msafara wake ukitokea katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe na kumwelezea kilio hicho.

Alisema baada ya kuwasikiliza aliagiza Wizara ya Maji kukamilisha mradi wa maji wa Shongo ili kumaliza tatizo hilo na kwamba utekelezaji ulianza na kukamilika ndani ya muda mfupi.

Baada ya kukamilika mradi huo, alisema maji katika mji huo si tatizo tena kwa maelezo kuwa yanapatikana kila eneo hali ambayo inawafanya wasimsahau kiongozi huyo.

"Tunamwombea alale mahali pema peponi. Sisi hapa Mbalizi hatuwezi kumsahau na tutaendelea kumwombea maana alitusaidia kupata maji ambayo ni mengi na ya uhakika.

Aliagiza siku moja tu lakini sisi tutafurahia miaka mingi," alisema Mwenizumba.

Mariam Mwabulambo ambaye ni mama lishe katika eneo la Soko Kuu alisema kabla ya kutekelezwa kwa mradi wa Shongo, walikuwa wananunua maji kwa gharama ya Sh. 400 mpaka 500 kwa dumu la lita 20.Alisema gharama hizo zilikuwa kubwa kiasi kwamba walikuwa wanapata faida ndogo kwenye biashara yao na kwamba wakati wa kiangazi ndio walikuwa wanapata shida zaidi.

Baada ya mradi huo kuanza kufanya kazi, alisema wananunua maji hayo kwa gharama ya kati ya Sh. 100 na 200 kwa vijana wanaotembeza huduma hiyo kwenye matoroli na kwamba wakienda wao wenyewe bombani kuchota wananunua ndoo tano za lita 20 kwa Sh. 100.

Alisema wanawake wa Mji huo hawatamsahau hayati Magufuli kutokana na kuwatatulia kero hiyo ambayo ilikuwa ya muda mrefu kwenye mji huo.

"Alipoagiza tulijua ni yale yale maneno ya wanasiasa lakini sasa tunaoga maji ya bomba kitu ambacho tulikuwa hatukijui. Tulikuwa tunakunywa maji ambayo hata hatujui usalama wake. Sasa hivi maji ni mengi mpaka hata watu binafsi wameanza kuvuta majumbani mwao," alisema Mwabulambo.

Hivi karibuni maofisa wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), walianza kuhamasisha wananchi kuomba kuingiziwa maji kwenye nyumba zao kwa madai kuwa maji ni mengi kuliko watumiaji.

Walisema kutokana maji hayo kuwa mengi na kasi kuwa kubwa, mabomba yameanza kupasuka na kusababisha upotevu mkubwa wa maji. Apirili 25 aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli alimwagiza aliyekuwa Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, kukamilisha mradi wa maji wa Shongo ili kumaliza tatizo la maji katika mji wa Mbalizi na akatishia kumtumbua endapo asingetekeleza.



Wananchi wa Kitongoji cha Mwashikamile, Kijiji cha Yara, wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, wakiwa kwenye mkutano wa kijiji uliojadili mambo mbalimbali ikiwamo migogoro ya ardhi kati yao na wawekezaji, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Busekelo yakumbwa uhaba vituo vya afya

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

LICHA ya serikali kuhamasisha ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya kwenye kila kata nchini, kata nane za Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe bado hazijaanza hata hatua moja ya kujenga vituo hivyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busokelo, Eston Ngilangwa, alisema halmashauri yake ina jumla ya kata 13 lakini miongoni mwake kata nane hazijaanza ujenzi wa vituo vya afya.

Akifafanua zaidi, Ngilangwa alisema kata mbili pekee ndizo zimeshakamilisha ujenzi wa vituo vya afya huku kata nyingine nne zikiwa tayari zimeshaanza ujenzi.

Vilevile alisema halmashauri hiyo ina vijiji 56 lakini kati ya hivyo ni 24 ambavyo vina zahanati zinazofanya kazi na vingine bado havina zahanati wala havijaanza ujenzi na vijiji 12 vimeanza ujenzi.

"Tunaendelea kuwahamasisha wananchi kushiriki kwenye ujenzi wa vituo hivi vya kutolea huduma za afya kwenye maeneo yao ili kusogeza huduma hiyo muhimu kwenye makazi yao," alisema Ngilangwa.

Hivi karibuni, wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyata, alisema mkoa huo una kata 179 na kubainisha kwamba kata 129 hazina vituo vya afya na hazijaanza ujenzi.

Pia alisema mkoa huo una Vijiji 714 lakini ambavyo vina Zahanati zinazofanya kazi ni 282 huku 242 vikiwa bado havijaanza kabisa ujenzi wa zahanati hizo.

Hata hivyo alisema Mkoa mzima wa Mbeya, una vituo vya kutolea huduma za afya 352 zikiwemo zahanati 297, vituo vya afya 35 na Hospitali 20.

# Miundombinu iliyoharibiwa kuboreshwa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI wilayani Kyela imeahidi kuboresha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko katika Kata za Mababu na Matema ili wananchi waendelee kupata huduma muhimu za kijamii.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Claudia Kitta, alitoa kauli hiyo alipofanya ziara ya kutembelea maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko hayo yaliyosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha katika maeneo ya Halmashauri za Rungwe na Busokelo.

Mafuriko hayo yalisababisha uharibifu kwenye miundombinu ya barabara, madaraja, makazi ya watu pamoja na kusomba mifugo hasa ng'ombe, mbuzi na nguruwe.

Kitta alisema serikali itahakikisha inashughulikia maeneo yote yaliyoathirika na kuyarekebisha mapema ili kuepuka wananchi wa maeneo hayo kuathirika kwa kukosa huduma muhimu za kijamii na kiuchumi.

"Tutakaa na wataalamu kujadili namna bora ya kurejesha miundombinu hii, ikiwezekana tutatenga bajeti maalumu ili kujenga miundombinu hii hasa barabara na madaraja, niwape pole sana wakazi wa maeneo haya kwa tatizo hili," alisema Kitta.

Alisema daraja muhimu lilikuwa limebomoka ambalo ndilo linaziunganisha kata hizo mbili na miji ya Ipinda na Kyela ambako ndiko wananchi wa maeneo hayo wanategemea kupata huduma muhimu.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Mababu, Rashid Yahya, alisema mwanzoni mvua ilikuwa inanyesha ya kawaida lakini Machi 30 ilikuwa kubwa na ndiyo iliyosababisha maafa.

Yahya aliiomba serikali kujenga miundombinu ya kudumu hasa madaraja kwa maelezo kuwa Wilaya hiyo huwa inakumbwa na mafuriko karibu kila mwaka kutokana na kuwa bondeni na kwamba mvua zinazosababisha mafuriko hayo huwa zinanyesha katika Wilaya ya Rungwe.

Alisema huwa ni vigumu kwa wananchi wa maeneo hayo kutabiri kwamba wanaweza wakakumbwa na mafuriko kutokana na wakati mwingine kutokea wakati katika maeneo yao jua linawaka.

"Kama mnavyoona madaraja yetu mengi hayawezi kuhimili maji mengi, tunaomba ikiwezekana tujengewe madaraja ya kisasa ili hata maji yakiwa mengi yasisombe na kukwamisha shughuli zetu," alisema Yahya.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Katumba katika Kata ya Mababu, Lwimiko Anyosisye, alisema pamoja na kwamba mafuriko hayo yalikuwa makubwa lakini hayakuleta madhara sana kwa binadamu kama ilivyowahi kutokea miaka mingine.

Alisema mwaka 2019 yalitokea mafuriko makubwa ambayo yalisababisha maafa kwa kuua watu, kuharibu miundombinu mbalimbali zikiwamo nyumba za watu, barabara, shule na kusomba mazao.





Baadhi ya wananchi, wanafamilia na viongozi wa serikali wakijumuika katika hafla ya kumuombea dua marehemu Maalim Seif Sharif Hamad, iliyofanyika kijijini kwao Mtambwe Njali-Mkoa wa Kaskazini Pemba jana, ikiwa ni utaratibu uliowekwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kuwaombea dua viongozi waliotangulia mbele ya haki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Familia kumuombea dua marehemu Maalim Seif

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

FAMILIA ya marehemu maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, imeipongeza Serikali ya Mapinduzi kwa kutenga siku maalum ya kumuombea dua mpendwa wao kama sadaka yake kwa yale mema aliyowafanyia wananchi katika uhai wake.

Akizungumza kwa niaba ya familia hiyo, Bakar Sharif Hamad, alisema Serikali ya Mapinduzi iliguswa kwa kuondokewa na kiongozi huyo aliyekuwa mstari wa mbele katika kupigania haki za wananchi.

"Lilioandikwa na Mwenyezi Mungu haliwezi kuepukika na kilichobakia ni kumkumbuka kwa duwa," alisema kaka wa Maalim Seif.

Alisema tangu kifo hicho Machi 17, mwaka huu, serikali imekuwa pamoja nao kuanzia ugonjwa na mpaka kifo na wanafamilia na inawapa faraja kuona kuwa pamoja na kuondoka Maalim Seif, lakini serikali bado inamthamini kwa kiasi kikubwa.

"Sisi wanafamilia hatuna budi kutoa shukrani zetu kwa serikali kwa kumjali mwenzao huyu tokea ugonjwa hadi kifo chake na sisi tumepata faraja kuona kila siku mmekuwa pamoja na sisi," alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Suleiman Massoud Makame, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika shughuli hiyo ya dua, alisema chakula cha maiti ni dua na ndio wananchi wapo katika kumtakia marehemu hatima njema na kumuombea kwa Mungu amsamehe makosa yake na amuepushie kila zito juu yake.

Aliwahakikishia wananchi kuwa jambo hiyo litakuwa endelevu na serikali imetenga siku maalumu ya kuwaombea dua viongozi wakuu wa serikali waliotangulia mbele ya haki kila mwaka ikifika muda huo litatendeka.

"Leo tumekusanyika hapa kumuombea dua mwenzetu huyu kwa vile ndio chakula chake kwa sasa, na tunamuomba Allah azidi kumuweka katika mahala pema na sisi tulioko duniani atupe hatima njema na watokee wengine watuombee dua kama hivi tunavyomuombea mwenzetu," alisema.

Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwaombea dua viongozi wake wakuu waliotangulia mbele ya haki kila ifikapo mwezi wa Aprili ya kila mwaka kwa kuungana na wanafamilia wa marehemu hao katika maeneo mbalimbali.

Kabla ya dua hiyo pia kulikuwa na ya kumuombea aliyekuwa Rais wa Zanzibar Aboud Jumbe, Idrisa Abdulwakil na aliyekuwa Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk Omar Juma na jana imehitimisha kwa kusomea dua Rais wa kwanza wa Zanzibar Hayati Abeid Amani Karume dua hiyo itasomwa Ofisi kuu za CCM Kisiwandui.

## Baa, nyumba za kulala wageni zafungwa kwa kukiuka sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Magharibi B Unguja imefanya ziara ya kukagua baa pamoja na nyumba za kulala wageni zinazofanya biashara kinyume na utaratibu na kutokuwa na leseni za biashara hizo.

Akizungumza baada ya ziara hiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Magharibi B ambaye pia ni Mkuu wa wilaya hiyo, Hamida Mussa Khamis, alisema katika ziara hiyo wamezifunga baa mbili ambazo zinaendesha biashara kinyume na sheria.

Baa zilizofungiwa ni Kwa Mbovu na Mchichuma zilizopo Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar.

Alisema pia wamelifungia duka la kuuzia vivywaji lililopo Bweni Kisima mbaazi na nyumba ya kulala wageni Promise iliyopo Bweni Kibiti, kutokana na kukiuka utaratibu wa uendeshaji wa biashara hiyo ikiwamo kutokuwa na leseni.

Alisema kila mwananchi anaruhusiwa kufanya biashara yoyote ya halali kwa kufuata sheria na taratibu ikiwamo kukata leseni katika mamlaka husika ili kuepuka usumbufu katika biashara yake.

Alisema kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ina wajibu wa kusimamia pale inapoona sheria na taratibu zinakiukwa na kusababisha athari kwa wananchi wa maeneo husika.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Manispaa ya Magharibi B Unguja, Ali Abdalla Natepe, aliwataka wafanya biashara hasa za vileo kufuata utaratibu wa kukata leseni za biashara hizo ili kuepuka usumbufu pamoja na kuipatia kodi serikali.

# Wananchi wahakikishiwa fidia miradi mikubwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewahakikishia wananchi na wakulima waliomo kwenye miradi mikubwa inayoanzishwa kwamba serikali iko makini kulipa fidia ya mali zao ili miradi hiyo iweze kuleta faida kwao na serikali yenyewe.

Akizungumza jana na wananchi na wakulima wa Kijiji cha Dodo, Jimbo la Chambani waliyoonyesha hofu ya malipo ya fidia ya mali zao baada ya kuutembelea mradi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji, alisema mtathmini Mkuu wa Serikali ameanza uchambuzi wa kazi hiyo ili kila mwananchi mwenye haki alipwe fidia yake.

Hata hivyo, wakati akiwaomba wananchi wa Dodo wasisite kutoa taarifa pale wanapobaini changamoto zinazojichomoza kwenye mradi huo, aliwatahadharisha kwamba serikali haitakuwa tayari kumlipa fidia mtu asiyehusika kwa kutumia ujanja utakaobainika.

Hemed aliwaeleza wananchi hao kwamba serikali imekuwa na nia safi ya kustawisha maisha ya wananchi wake na kufikia uamuzi wa kuanzisha miradi mikubwa.

Aliutaka uongozi wa Wizara ya Kilimo kupitia wahandisi wake kuharakisha utekelezaji wa mradi huo wa umwagiliaji uliokusudiwa kuanza mapema mwaka 2019.

Aliwataka wahandisi wa mradi huo kuwapatia fursa za ajira vijana wa vijiji vinavyouzunguka mradi huo kwa zile kasi zisizohitaji taaluma kubwa.

Akisalimiana na wananchi wa Kijiji cha Chokocho wanaojishughulisha na kilimo cha mwani baada ya kupokea changamoto zao, alisema wakulima wa mwani lazima waendelee kupata kipato sahihi kulingana na nguvu wanayotumia wakati wa kuendeleza kilimo hicho.

Alitoa rai kwa kampuni isiyochangia vifaa pamoja na mafunzo kwa ajili ya utayarishaji wa ukulimwa wa mwani inastahiki kupigwa marufuku ya kutonunua zao hilo kutoka kwa wakulima.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za serikali za wilaya ya mkoani ndani ya mwezi Julai 2020 hadi Machi 2021, Mkuu wa wilaya hiyo, Issa Juma Issa, alisema huduma za kiuchumi na ustawi tayari zimewafikia wananchi kwa zaidi ya asilimia 80.

Issa alizitaja huduma hizo zilizoleta mafanikio ni pamoja na huduma za umeme, utatuzi wa mogogoro ya ardhi pamoja na uokoaji wa zao la karafuu uliosababisha kununuliwa kwa tani 97.87 za karafuu zenye thamani ya Sh. bilioni 1.3. Hata hivyo, alisema zipo changamoto kubwa zinazoleta kero ndani ya wilaya hiyo akitolea mfano kesi za udhalilishaji pamoja na kupungua kwa ufaulu wa shule za sekondari licha ya kupanda kwa ufaulu kwa zile shule za msingi.

Wakati huo huo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, alitembelea Hospitali ya Wilaya ya Mkoani ya Abdullah Mzee, kuangalia mazingira halisi ya utoaji huduma za afya ambazo hakuridhika nazo.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

Nafasi za Kazi ualimu diploma science/math/IT 0715382833

Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**SULILA S. KANAGANA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1424/0151** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **SOGESCA SEKONDARI** mwaka **2015.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/5121/2019.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALFRED MATHIAS MBOYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina Toyota-Corola, yenye namba za usajili **T.739 BPH.** Chassis namba **NZE1203000427** na Engine namba **2nzfe1533891.** Kwa yeyote atakayeiona kadi hiyo anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi cha karibu. Taarifa Polisi.**MUH/RB/958/2021.**

**THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2012**
**MUMA ENTERPRISES CO. LTD**

## TAARIFA KWA UMMA

Tunapenda kutoa tangazo kwa umma kuwa Kampuni ya MUMA ENTERPRISES CO. LTD yenye usajili Na. 98004 iliyo na Ofisi zake maeneo ya Jiji la Dar es salaam, inafungwa kwa hiyari ya wanahisa wenyewe. Hivyo tunaomba kama kuna Taasisi au mtu yeyote ana madai awasiliane na sisi kupitia anwani ifuatayo, ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kutolewa tangazo hili.

**Mkurugenzi**
**MUMA ENTERPRISES CO. LTD**
**P.O. Box 21363**
**Dar es salaam.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF GEITA**
**AT GEITA**
**CRIMINAL APPEAL No. 23 OF 2020**
**MOSES NAFTARI............APPEEALLANT**
**VERSUS**
**EMMANUEL PAILEMBO...RESPONDENT**

## NOTICE OF DATE FOR MENTION

TAKE NOTICE THAT, the above case has been fixed for Mention on the 12 day of April, 2021 at 09.00 am. YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

GIVEN UNDER my hand and the SEAL of the Court this 06 day of April, 2021.

RESIDENT MAGISTRATE

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Sudan yatangaza hali ya hatari

**Darfur,** SUDAN

SUDAN imetangaza hali ya dharura Magharibi mwa Darfur kufuatia mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yaliyosababisha watu 40 kufariki.

Kutokana hali hiyo maelfu ya watu waliyakimbia makazi yao.

Juzi, Umoja wa Mataifa (UN), ulisema watu wapatao 40 waliuawa na zaidi ya watu 50 walijeruhiwa katika ghasia zilizotokea siku ya Jumamosi wiki iliyopita, kati ya makundi ya kiarabu na wasio katika makundi ya jamii ya kiarabu katika mji wa El Geneina.

Milio ya risasi ilisikika katika maeneo ya jirani ya Hay Al Jabal na Al Jamarik siku ya Jumatatu mchana, UN, ilisema. Hali ya usalama bado inatia hofu katika mji huo kwa kuwa kila upande unachochea wanajeshi wake, UN iliongeza.

Operesheni mbalimbali za msaada zimesitishwa mpaka hali irejee kuwa nzuri. Mji huo umekuwa eneo la kupokea misaada na zaidi ya watu 700,000 wameathirika na mgogoro huo, kwa mujibu wa UN.

Januari, mgogoro kati ya jamii ya Massalit na jamii ya kiarabu ulisababisha vifo vya watu wapatao 129 na watu zaidi ya 108,000 kukimbia makazi yao na baadhi wakiishi katika shule na maeneo ya vituo vya afya. **BBC**

## Wenye chanjo corona pekee kuhiji Mecca

**Riyadh,** SAUDI ARABIA

MAMLAKA za nchini Saudi Arabia zimesema watu waliopata chanjo ya corona pekee, ndio wataruhusiwa kufanya ibada ya Hija mwaka huu, Mecca.

Wizara ya Hija na Umrah, ilitoa taarifa kuwa watu waliopata chanjo ndio watakuwa na vigezo vya kujihi mwaka katika mji mtakatifu wa Mecca. Wizara hiyo ilisema pia kuwa itazingatia taratibu zote za kujikinga dhidi ya maambukizi ya corona.

Haijawekwa wazi kama sera hiyo itaendelea mpaka wakati wa Hija kuu baadae mwaka huu.

Saudi Arabia iliripoti kuwa na maambukizi ya virusi vya corona zaidi vya zaidi ya watu 393,000 na zaidi ya vifo 6,700 vinavyotokana na virusi hivyo. Wizara ya afya ya taifa hilo ilisema watu zaidi ya milioni tano wamepata chanjo dhidi ya corona, katika taifa lenye watu zaidi ya milioni 34.

Mwezi uliopita mfalme Salman alimbadilisha waziri wa Hija, alafu mwezi mmoja baadae ilifanyika Hija ndogo katika mfumo mpya wa kihistoria kutokana na changamoto ya virusi vya corona. **BBC**

# Ripoti: Huawei yajizatiti kuboresha huduma kwa jamii

**SHENZHEN,** China

KAMPUNI ya Huawei imetoa ripoti yake ya mwaka 2020 ambayo pamoja na mambo mengine, imeonesha mapato yatokanayo na mauzo kwa mwaka uliopita yalifikia kiasi cha CNY bilioni 891.4 sawa na ukuaji wa asilimia 3.8 wa mwaka hadi mwaka, huku faida yake kuu ikifika kiasi cha CNY bilioni 64.6 sawa na ukuaji wa asilimia 3.2 wa mwaka hadi mwaka.

Aidha ripoti hiyo imebainisha kuwa ukuaji wa kampuni hiyo ulikuwa wa polepole licha ya ufanisi wake kibiashara kwenda sambamba na makadirio.

"Licha ya changamoto za kiutendaji zilizosababishwa na vikwazo vya Marekani mnamo 2019 na 2020, Huawei imeendelea kualika Kampuni ya ukaguzi wa mahesabu ya KPMG kukagua taarifa zake za kifedha kwa uhuru na kwa malengo."

"Hati iliyotolewa na KPMG ni maoni ya kawaida ya ukaguzi usiobadilishwa. Haijalishi hali ni nini, tutaendelea kukumbatia uwazi kwa kufichua data za utendaji kwa serikali, wateja, wauzaji, wafanyakazi, na washirika," alisema Ken Hu, Mwenyekiti wa Huawei.

**Tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na wateja wetu na washirika wetu kusaidia maendeleo ya kijamii, ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu.**

Mwaka wa 2020, biashara ya mawasiliano ya simu ya Huawei iliendelea kuwa thabiti kiutendaji kupitia mitandao yake zaidi ya 1,500 katika nchi na maeneo zaidi ya 170, ambayo ilisaidia katika utoaji wa huduma za simu, mafunzo ya mtandaoni na manunuzi kupitia mtandaoni wakati wote wa mapumziko ya COVID-19 (lockdown).

Kufanya kazi pamoja na watoa huduma za mawasiliano kote nchini, kampuni hiyo ilisaidia kutoa uzoefu bora wa kushikamana na kusonga mbele na zaidi ya miradi 3,000 ya uvumbuzi wa 5G katika tasnia zaidi ya 20 kama uchimbaji wa makaa ya mawe, uzalishaji wa chuma, bandari na viwanda.

Katika mwaka uliopita, biashara ya Huawei iliongeza juhudi za kukuza suluhisho za ubunifu wa mazingira kwa tasnia tofauti na kuunda ekolojia ya kidijitali ambayo inastawi juu ya uundaji wa pamoja na mafanikio ya pamoja. Wakati wa janga la COVID 19, Huawei ilitoa utaalamu wa kiufundi na suluhisho ambazo zilikuwa muhimu katika vita dhidi ya janga hilo.

"Katika mwaka uliopita tumeendelea kuwa imara katika kipindi chenye changamoto," alisema Ken Hu,

"Tumeendelea kubuni ili kujenga thamani kwa wateja wetu, kusaidia kupambana na janga hilo, na kusaidia kufufua uchumi na maendeleo ya kijamii kote ulimwenguni. Pia tumechukua fursa hii kukuza zaidi shughuli zetu, na kusababisha utendaji ambao kwa kiasi kikubwa ulikuwa sambamba na mpango wetu".

"Tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na wateja wetu na washirika wetu kusaidia maendeleo ya kijamii, ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu," aliahidi.



Gereza la Owerri nchini Nigeria, ambalo lilishambuliwa na waasi na kusababisha zaidi ya wafungwa 1,800 kutoroka. Kundi linalotaka kujitenga la wenyeji wa Biafra wenye silaha linadaiwa kushambulia jela hiyo, jana. **PICHA: BBC**

# Wafungwa 1,800 watoroka Nigeria

**Imo,** NIGERIA

ZAIDI ya wafungwa 1,800 wametoroka Kusini mwa Nigeria, baada ya kundi la watu wenye silaha kuishambulia jela ya Owerri katika moja ya uvamizi mkubwa zaidi wa gereza kwenye kanda ya Afrika Magharibi.

Maofisa wa idara ya magereza walisema washambuliaji waliingia kwenye jela hiyo iliyopo katika jimbo la Imo wakitumia milipuko na kufyetua bunduki na kisha kuwafungulia wafungwa waliokuwamo.

Washambuliaji ambao hadi sasa bado hawajafahamika waliwasili kwenye viunga vya gereza hilo wakiwa kwenye mabasi na magari ya wazi na maofisa wa Nigeria walisema idadi kamili ya wafungwa waliotoroka bado haijafahamika.

Rais Muhammadu Buhari wa Nigeria alilitaja tukio hilo kuwa shambulizi la kigaidi lililofanywa na waasi na ameitolea wito vyombo vya dola kuwakamata waliohusika pamoja na wafungwa waliotoroka. **DW**

# MOYES: LINGARD AMELETA TOFAUTI




**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa West Ham United, David Moyes, amemsifia Jesse Lingard, ambaye amehusika kwenye mechi nyingi zaidi Ligi Kuu England kuliko mchezaji yeyote tangu kuanza kuwachezea 'Wagonga Nyundo' hao.

Lingard alifunga bao la ufunguzi wakati West Ham ikishinda mabao 3-2 Jumatatu ugenini dhidi ya Wolverhampton na kukifanya kikosi cha Moyes kujikita nafasi ya nne na kuipiku Chelsea.

Akiwa anacheza kwa mkopo kutoka Manchester United, winga huyo amefunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho tatu tangu kuanza kuwachezea Wagonga Nyundo hao Februari 3.

"Kasi ya Jesse ni kubwa na uwezo wake unaisaidia timu," alisema Moyes akiwaambia waandishi wa habari.

"Ameonyesha kuwa ni msaada kwa kikosi chetu na ninaamini ataweza kufanya vizuri zaidi."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anafurahia kiwango chake bora zaidi baada ya kukosa nafasi kule Old Trafford katika misimu ya hivi karibuni.

# Zidane amkana Mo Salah

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amefunguka juu ya tetesi zinazomhusisha, Mohamed Salah kutua Real Madrid.

Salah amekuwa katika vichwa vya habari wiki iliyopita baada ya kukiri kwamba yupo tayari kucheza nchini Hispania hapo baadaye.

Mshambuliaji huyo raia wa Misri kwa sasa anajaribu kuonyesha hisia zake za kuhama na kwenda kule Santiago Bernabeu wakati wa majira ya joto, lakini Zidane amepuuza kuhusishwa na kumhitaji mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, wakati wa mkutano na waandishi wa habari.

Alipoulizwa kama angependa kumfundisha Salah, bosi huyo wa Real Madrid aliwaambia waandishi wa habari: "Si mchezaji wangu.


"Nina wachezaji 25 hapa, kwa sasa mimi ni kocha wa Real Madrid na ninafurahia kila siku ya matukio.

Salah aliongeza ukubwa wa uvumi juu ya hatima yake kule Liverpool wakati wa mahojiano na gazeti la AS Desemba mwaka jana baada ya kusema anahitaji changamoto mpya katika ligi ya LaLiga.

"Nadhani Barcelona na Real Madrid ni klabu kubwa, nani anayejua kuwa nini kitatokea hapo baadaye," alisema.

Salah alijiunga na Liverpool mwaka 2017 kwa kitita cha pauni milioni 37akitokea AS Roma wakati wa dirisha la majira ya joto.

Amefunga mabao 120 katika michezo 193 tangu ajiunge na 'Wekundu' hao akisaidia kutwaa taji la Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya.






# Koeman: Clasico ni muhimu sana kwetu

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Ronald Koeman, amekubali kwamba mchezo unaokuja wa El Clasico ni mkubwa mno kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Miamba hao wa Catalunya wamepitwa pointi moja na vinara wa ligi, Atletico Madrid baada ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Real Valladolid, huku wakiwapita Real Madrid waliopo nafasi ya tatu kwa pointi mbili.

Atletico walipoteza pointi tano katika mechi nane zilizopita, ikiwamo ya kipigo cha bao 1-0 kutoka Sevilla, na kufungua mlango kwa mbio za ubingwa.

Barcelona watakuwa ugenini kucheza na Madrid Jumamosi, huku Atletico wakicheza na Real Betis waliopo nafasi ya tano.

"Nafikiri mara zote Clasico ni muhimu," alisema Koeman.

"Bila shaka, ni muhimu sana kwa sasa kwa sababu ya hali halisi ya ligi, sehemu tulipo na Real Madrid tunapigana dhidi ya Atletico Madrid kushinda msimu huu."

Barcelona itaingia kwenye mchezo wa El Clasico ikiwa na kiwango bora, ikiwa imeshinda mechi sita za LaLiga na kucheza 19 bila kufungwa.

Madrid haijafungwa kwenye mechi tisa kwenye ligi na wameshinda tatu za LaLiga zilizopita.

# Haaland hauzwi kwa namna yoyote

**DORTMUND,** Ujerumani

KLABU ya Borussia Dortmund imepanga kumbakisha Erling Haaland lakini watasikiliza ofa itakayokuja kwa Jadon Sancho, kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu Hans-Joachim Watzke.

Haaland amekua mchezaji lulu msimu huu na klabu za Ulaya zimepania kumsajili wakati wa majira ya joto baada ya kuwa na msimu bora wa 2020-21 pale kwenye dimba la Westfalenstadion.

Watzke amedai Dortmund haijafikiria kumuuza raia huyo wa Norway, lakini anakubali kwamba Sancho anaweza kuishia kuondoka kama atapata ofa inayofaa soko likifunguliwa.

"Hatuna mpango wa kumuuza. Tutazungumza hili na Erling, baba yake na wakala wake Mino Raiola," alisema Watzke akiiambia Goal na DAZN.

"Tunataka pia afurahi kukaa nasi, kuifungia BVB mabao mwakani, hakuna mpango mbadala."

Alipoulizwa kama Haaland na Sancho wote bado watakuwapo kwenye vitabu vya Dortmund msimu 2021-22, Watzke alijibu: "Sijihusishi na uwezekano, si mzuri."

"Jadon Sancho amekuwa nasi kwa muda mrefu zaidi kuliko Erling Haaland. Itakuwa lazima niongee na Jadon pia.

Sancho alikuwa katika nafasi kubwa ya kuuzwa mwaka jana, akitajwa kama chaguo namba moja kwa United wakati wa kutafuta winga wa kulia.

'Mashetani Wekundu' mwishowe walikataa kufika bei ya pauni milioni 100, lakini ripoti za hivi majuzi zimesema kuwa wanajiandaa kurudisha nia yao kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa England.




# BABA AMBAKIZA RAMOS MADRID




**MADRID,** Hispania

WAZAZI wa beki kisiki anayekipiga ndani ya kikosi cha Real Madrid, Sergio Ramos, wameamua kuvunja ukimya kuhusu hatma ya mtoto wao huyo.

Ramos amekuwa akitajwa kuwa anaweza kuondoka ndani ya kikosi hicho cha Madrid kinachonolewa na kocha, Zinedine Zidane. Jose Maria Ramos, baba mzazi wa Ramos amesema kuwa nyota huyo atabaki kikosini hapo.

"Ama hakika atasalia ndani ya Real Madrid ni suala ambalo familia imeamua hilo liwe namna hiyo."

Paqui Garcia ambaye ni mama mzazi wa Ramos amesema kuwa mwanaye atabaki Real Madrid.

Ramos mwenye umri wa miaka 35, amekuwa kwenye rada za timu nyingi Ulaya ikiwamo Machester United na PSG, wakati mkataba wake ukiwa unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu.

# *Rabiot sasa aingia rada za Chelsea*

**LONDON,** England

KIUNGO wa Juventus, Adrien Rabiot, ameripotiwa kuibuka kwenye rada za Chelsea kuelekea dirisha la uhamisho la msimu ujao wa majira ya joto.

Nyota huyo wa miaka 25, amecheza mechi 72 tangu alipowasili kule Turin kama mchezaji huru akitokea Paris Saint-Germain mwaka 2019.

Hata hivyo, wakati Juventus wakiwa kwenye mpango wa kupunguza mzigo wao wa mishahara ya wachezaji, nyota huyo amekuwa akihusishwa zaidi na kuondoka klabuni hapo.

Kwa mujibu wa Tuttomercato, Chelsea watatumia nafuu ya hali hii kujaribu kuwasilisha ofa yao ya kumsajili Rabiot.

Licha ya ukweli kuwa ana uhakika wa wachezaji kwa safu ya kati, kocha Thomas Tuchel anaweza kutarajia kufanya mabadiliko kidogo kupitia dirisha lijalo, na hii itakuwa ni moja ya fursa muhimu kwake ikiwa anataka Rabiot abadilishe hali ya hewa kwenye safu ya kiungo wa kati.

Kwa mujibu wa ripoti, Chelsea wanaunga tela kwa Everton na Manchester United ambao kwa pamoja wanatajwa kuwa wapo kwenye mbio za kuiwania saini ya staa huyo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA SASA ASHAURIWA KUMTEMA AUBAMEYANG

## Ni kutokana na kiwango, atakiwa kuanza kumpa nafasi Martinelli, ambaye....

**LONDON,** England

KOCHA mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta, ameshauriwa kumuweka benchi kwa muda mshambuliaji wake, Pierre Emerick Aubameyang na kuanzisha kikosi cha kwanza Gabriel Martinelli.

Ushauri huo umetolewa na mchezaji wa zamani wa kikosi hicho na mchambuzi wa michezo, Martin Keown kupitia gazeti la Daily Mail, kutokana na mwendo wa nahodha huyo kuwa wa kusuasua kikosini humo.

**Arteta ameongoza jumla ya mechi 50 akiwa Arsenal, lakini kiwango cha wachezaji wake kimekuwa kama gari bovu, huku ikitoka kuchezea kichapo cha mabao 3-0 kutoka Liverpool.**

Keown amesema ni lazima Arteta afanye uamuzi mgumu ya kumuweka kando kwanza Aubameyang na kumuanzisha kijana Gabriel kwa kuwa amekuwa na uwezo mkubwa.

Arteta baada ya kupoteza mbele ya Liverpool aliomba msamaha kwa mashabiki wa timu hiyo kwa kuwa alikuwa anaamini kwamba walikuwa na nafasi ya kupata pointi tatu muhimu.

## ZISIKUPITE

### WAKALA AKANA YA HAALAND

WAKALA wa mchezaji Erling Haaland, Mino Raiola, amekana tetesi kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, 20. ***(Goal)***

### IBRAHIMOVICH MKATABA MPYA

NYOTA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovich, 39, anatarajia kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja na klabu hiyo. ***(Sky Sports)***

### DE GEA TAYARI KUONDOKA

KIPA wa Hispania, David de Gea, 30, yupo tayari kuondoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

### ODEGAARD KUBAKI ARSENAL

ARSENAL wanataka kumbakiza kiungo, Martin Odegaard, 22, klabuni hapo ambaye anacheza kwa mkopo akitokea Real Madrid. ***(AS)***

### HAALAND KUBAKIZWA

MTENDAJI Mkuu wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke, amesisitiza kuwa klabu yake inataka kumfanya Erling Haaland kuwa na furaha zaidi klabuni hapo ili aweze kusalia mpaka msimu ujao. ***(Dazn via Mirror)***

### GUARDIOLA NA USAJILI CITY

KOCHA wa Manchester United, Pep Guardiola, amesema wanaweza kuamua kutumia zaidi ya pauni milioni 100 kwa ajili ya mchezaji mmoja siku za usoni, lakini ameendelea kuwa na kigugumizi juu ya tetesi kuhusu klabu yake kuhusishwa na Erling Haaland. ***(Sky Sports)***

### HALI NGUMU USAJILI BARCA

BARCELONA itaendelea na mipango yake ya kumuwania mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, baada ya kukutana na wawakilishi wake wiki iliyopita, lakini vyanzo katika klabu hiyo vinasema kuwa itakuwa “vigumu sana” kutekeleza azma yao. ***(ESPN)***

### ZIDANE AVUNJA UKIMYA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amevunja ukimya kuhusu tetesi za uhamisho zinazomhusisha mshambuliaji wa Misri na Liverpool, Mohamed Salah, 28, kuhamia Bernabeu. ***(Liverpool Echo)***

### FOYTH KUPEWA MKATABA

KLABU ya Villarreal ina matumaini ya kumsajili mlinzi, Juan Foyth, 23, kwa mkataba wa kudumu kutoka Tottenham. ***(Football Insider)***

### DI MARIA AMTAKA MESSI

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Angel di Maria, 33, amesema itakuwa “vizuri sana” kucheza na raia mwenzake wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, wakati huu kukiwa na mashaka kuhusu mustakabali wake ndani ya Barcelona. ***(AS)***

## Bunge laipongeza Simba Mabingwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeipongeza Klabu ya Simba kwa kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF), ikiwa ni siku chache baada ya kuibanjua AS Vita ya DR Congo kwa mabao 4-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akitoa pongezi hizo jana bungeni jijini Dodoma, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema kuna wabunge yawezekana hawajaelewa uzito wa ushindi huo wa Simba.

"Ni jambo ambalo sisi kama taifa tunapaswa kuungana kuwatia moyo wachezaji wetu na klabu yetu iendelee kufanya vizuri kwa sababu inapata fursa ya kuitangaza nchi yetu vizuri," alisema.

Dk.Tulia alisema "Naamini mashabiki wa Yanga wataungana nami katika pongezi hizi kwa klabu ya Simba."

## Msajili ataka marekebisho mapya katiba ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MSAJILI wa Vyama vya Michezo Zanzibar, Abubakar Lunda, ameliagiza Shirikisho la Soka visiwani hapa (ZFF), kuwasilisha mapema ofisini kwake mabadiliko ya katiba waliyofanyia marekebisho katika mkutano mkuu uliopita.

Akizungumza na gazeti hili jana visiwani hapa, msajili huyo alisema kwa mujibu wa sheria za vyama vya michezo, mabadiliko yote ya katiba ya vyama hivyo yanapaswa kupelekwa ofisini kwake kupitiwa pamoja na kutoa ruhusa ili yaanze kutumika. Alisema ZFF katika mkutano wake mkuu uliopita, walifanya marekebisho madogo ya katiba yao katika vipengele mbalimbali, hivyo ni vema yakapelekwa ofisini kwake ili yaweze kupata baraka na kuanza kutumika rasmi.

Aidha, alikumbusha kuwa katika uchaguzi wa shirikisho hilo ambao unatarajiwa kufanyika baadaye mwezi huu, ZFF itatumia katiba hiyo ambavyo imelifanyiwa marekebisho, hivyo ni vema wakawasilisha marekebisho hayo ili kupata baraka ya kutumika.

# ONYANGO AZITISHA TIMU LIGI YA MABINGWA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

BEKI anayesemekana kuwa ni mmoja kati ya mabeki bora kwa sasa Afrika, Joash Onyango, amesema hawaiogopi timu yoyote ile inayocheza Ligi ya Mabingwa Afrika na kwamba wao kama wachezaji kazi yao ni kupambana na si kuangalia jina la klabu.

**Onyango ambaye Simba ilimsajili kutoka Gor Mahia msimu uliopita, amesema lengo lao la kwanza ni kumaliza mechi za Kundi A wakiwa vinara ambalo wamelitekeleza, lakini la pili ni kumaliza bila kupoteza.**

"Wala usidhani tunakwenda kucheza na Al Ahly kwa kukamilisha ratiba kwa sababu tumepita. Tunakwenda kumalizia mechi ya kundi letu tukiwa hatujapoteza kwa sababu ni moja kati ya malengo tuliojiwekea," alisema Onyango ambaye usajili wake ndani ya Simba ulibezwa na baadhi ya mashabiki kwa madai kuwa ana umri mkubwa kutokana na mwonekano wake.

Simba ilitarajiwa kusafiri jana kwenda nchini Misri kukamilisha mechi zake za Kundi A, ikiwa tayari imeshapata tiketi ya kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini pia ikiongoza kundi kwa pointi 13, hivyo hata ikipoteza mechi ya mwisho itakayopigwa Ijumaa wiki hii, itaendelea kuwa kinara.

"Kwa sasa hatuiogopi timu yoyote, siyo kwa sababu tupo vizuri au tumekuwa tukipata matokeo mazuri, lakini kwa hatua ambayo tumefika ni kwamba timu zote ni nzuri, huwezi kusema hii ni bora kuliko hii. Sisi wote tulioingia robo fainali ni bora, kwa hiyo muhimu ni kwamba wachezaji wote tunajua majukumu yetu, ni kupambana tu ili kuipatia timu ushindi na kuipa klabu mafanikio." Alisema Onyango ambaye kwa sasa amekuwa kipenzi cha mashabiki wa Simba.

Simba itacheza na mshindi wa pili kutoka B, C ama D kwenye hatua ya robo fainali baada ya droo ya michuano hiyo kuchezeshwa Aprili 30, mwaka huu.

Kuhusu zile ndevu zake kama mzee, amesema kuwa ataziweka mara tu atakaporejea kutoka nchini Misri.

"Nilisema siku chache hivi kuwa nitazirudisha, nadhani nikitoka Misri nitazirudisha zile ndevu zangu nyeupe," alisema huku akiangua kicheko.




Wachezaji wa Fenerbahçe wakimpongeza mshambuliaji wa timu hiyo, Mtanzania Mbwana Samatta (katikati), baada ya kuifungia bao pekee wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Denizlispor katika mchezo wa Ligi Kuu Uturuki uliopigwa Uwanja wa Ülker Fenerbahçe Şükrü Saracoşlu Spor Complex jijini Istanbul juzi. **PICHA: MTANDAO**

# *Kombe la FA Zanzibar sasa baada ya Ramadhani*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar maarufu Kombe la FA, imepangwa kuanza kuchezwa baada ya kumalizika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Awali Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kupitia kwa Kamati yake ya Mashindano, ilipanga michuano hiyo iliyopo katika hatua ya 16-bora, kuanza kuchezewa leo Aprili 7, lakini sasa imesogezwa mbele.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya ZFF ambaye pia ni mratibu wa michuano hiyo, Haji Issa 'Kidali', alisema kusogezwa mbele kwa michuano hiyo kumetokana na kupisha michezo ya viporo vya Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema hatua hiyo imefikiwa kutokana na timu nyingi zilizofanikiwa kutinga hatua 16-bora zinatoka Ligi Kuu, hivyo ratiba ya Kombe la FA imeingiliana na ya Ligi Kuu, hivyo wakaona ni vema michuano hiyo ikachezwa baada ya kumalizika kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Kidali alisema sababu nyingine iliyochangia mabadiliko hayo ya ratiba ni muda mdogo uliopo wa kucheza ligi hiyo ikilinganishwa na idadi ya michezo waliyonayo katika hatua hiyo ya 16-bora.

Alisema Mwezi wa Ramadhani unatarajiwa kuanza Aprili 13, mwaka huu lakini itategemeana na muandamo wa mwezi, hivyo kwa siku zilizobaki haitatosha kucheza Ligi Kuu pamoja na michuano hiyo FA.

Aidha, Kidali alizitaka klabu zote zilizoingia hatua hiyo kuelekeza maandalizi yao katika michezo ya Ligi Kuu kwa sasa na baada ya Ramadhani wajiandae na michuano hiyo ya FA.

# Michezo

Jumatano Aprili 7, 2021

Nipashe




Arteta ashauriwa kumtema Aubameyang UKURASA 22

TUPO TAYARI...



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi ya mwisho katika Uwanja wa Simba Mo Arena, kabla ya kukwea pipa jana kuelekea Misri tayari kwa mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayopigwa Ijumaa wiki hii. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA WAANIKA MBINU KWENDA KUIUA AL AHLY

## ●●● Gomes ataja jeshi lake asema wanachotaka ni ushindi, wachezaji morali juu wafunguka...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa soka nchini, Simba, wamekwea pipa kuelekea Misri jana, tayari kwa mechi yao ya mwisho ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly, huku wakieleza mbinu walizozitumia ambazo zinaweza kuwapa matokeo chanya ugenini dhidi ya wapinzani wao hao.

**Simba ambayo ipo kileleni ikiwa na pointi 13 ikifuatiwa na Al Ahly yenye alama nane, kisha AS Vita ambayo ina pointi nne na Al-Merrikh ikiburuza mkia na pointi zake mbili, hata kama ikipoteza keshokutwa, Ijumaa, itaendelea kuwa kinara wa kundi hilo ikifuatiwa na Wamisri hao.**

Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, amesema kuwa pamoja na kufuzu hatua ya robo fainali huku wakiwa vinara wa kundi lao, watashuka dimbani nchini Misri wakiwa na lengo moja tu la kupata matokeo.

Gomes alisema, ushindi dhidi ya Al Ahly ugenini utazidi kukiimarisha kikosi chake na kukijengea kujiamini kuelekea hatua inayofuata, hivyo wataukabili mchezo huo wakiwa na kikosi kamili kama walivyofanya kwenye mechi nyingine.

Kwa upande wa beki wa kati wa timu hiyo, Joash Onyango, amesema hawaiogopi timu yoyote ile inayocheza Ligi ya Mabingwa Afrika na kwamba wao kama wachezaji kazi yao ni kupambana na si kuangalia jina la klabu.

Onyango alisema: "Wala usidhani tunakwenda kucheza na Al Ahly kwa kukamilisha ratiba kwa sababu tumepita. Tunakwenda kumalizia mechi ya kundi letu tukiwa hatujapoteza kwa sababu ni moja kati ya malengo tuliojiwekea."

Lakini Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez yeye aliwatoa hofu mashabiki wa timu hiyo akisema, benchi la ufundi lilipata muda zaidi ya mara mbili wa kufanyia kazi mechi dhidi ya Al Ahly, hivyo wanakwenda Misri wakiwa na lengo la kupata matokeo.

"Tupo tayari kiintelijensia, msimu huu nimewekeza sana katika 'analysis' [uchambuzi], tumemuajiri mtu kwa kazi hiyo, leo tunaweza kufuatilia mchezaji fulani na kujua huyu ni hatari, na kutoa maagizo kwa wachezaji wetu namna ya kumkaba, mpira unaendeshwa kisayansi, kila kitu kinakwenda kwa takwimu.

"Tunapoelekea mechi yetu na Al Ahly tupo tayari, kwani wakati wa mapumziko ya kupisha Kalenda ya Fifa, walimu wetu walipata muda wa kutosha kuwachambua sana wapinzani wetu na ninaweza kusema wamefanya maandalizi mara mbili zaidi kuifuatilia na waliifanyia kazi sana

"Itakuwa ni mechi ngumu maana Al Ahly ni timu kubwa hatuwezi kwenda tukiwa tunajiamini sana ila tumefanya maandalizi makubwa," alisema Barbara.

Simba iliondoka jana saa 9:25 alasiri ikiwa na msafara wa wachezaji 25 na viongozi 12 kwa ndege ya Shirika la Ngege la Emirates ambapo ilipumzika Dubai na leo majira ya saa 4:05 itatua Cairo, Misri tayari kwa mchezo huo utakaopigwa Ijumaa.

Wachezaji walioondoka katika msafara huo ni makipa: Aishi Manula, Beno Kakolanya na Ally Salim, wakati mabeki wakiwa ni Shomari Kapombe, Joash Onyango,Pascal Wawa, Ibrahim Ame, Erasto Nyoni, Gadiel Michael, Mohamed Hussein, Kennedy Juma na David Kameta,

Viungo ni Jonas Mkude, Rally Bwalya, Said Ndemla, Mzamiru Yassin, Luis Miquissone, Hassan Dilunga, Clatous Chama, Bernard Morrsion, Francis Kahata na Taddeo Lwanga, wakati washambuliaji wakiwa ni Meddie Kagere, John Bocco, Ibrahim Ajib na Kope Mugalu.

# Yanga kumtetea Mwakalebela TFF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imepinga adhabu iliyotolewa na Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) ya kumfungia Makamu Mwenyekiti wake, Fredrick Mwakalebela, kutojihusisha na masuala ya mpira wa miguu ndani na nje ya nchi pamoja na faini la jumla ya Sh. milioni saba kwa makosa ya kimaadili.

Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Haji Mfikirwa, amesema wao kama viongozi wa Yanga hawajaridhishwa kabisa na adhabu hiyo, hivyo wanajiandaa kupinga hukumu hiyo kwa njia zilizowekwa kwa kikatiba na kistaarabu.

Hata hivyo, alisema kuwa tamko rasmi la klabu hiyo litatolewa na Mwenyekiti, Dk. Mshindo Msolla kutokana na jambo lenyewe linamhusu makamu mwenyekiti.

"Msimamo rasmi wa klabu utatolewa na Mwenyekiti kwa sababu jambo linamhusu makamu mwenyekiti. Kwa ukubwa huo ni busara likaongelewa na mwenyekiti, lakini sisi kama klabu kwa haraka haraka hatujaridhishwa na uamuzi huo," alisema Kaimu Katibu huyo na kuongeza.

"Tunachoshangaa ni kwamba klabu ndiyo iliitisha mkutano na waandishi wa habari, hakuitisha yeye binafsi na hata tangazo wa mkutano lilitolewa na Klabu ya Yanga, ameongea kwa niaba ya klabu kwa kupewa baraka zote, sasa kwenye adhabu hiyo tumeona kamati inadai eti makamu mwenyekiti ndiyo ameitisha mkutano huo. Sasa kwa nini aadhibiwe kama yeye binafsi?" alihoji.

Kutokana na hali hiyo alisema kuwa wao kama klabu watakaa na kuipitia adhabu hiyo pamoja na kupata ushauri kwa sababu kamati hiyo siyo ya mwisho.

"Tutaona Katiba ya TFF inasemaje. Tutadai haki yetu kwa njia ya kistaarabu kabisa. Hapo siyo mwisho na sisi viongozi tutakuwa nyuma yake kwa sababu alikuwa akiisemea klabu na si mambo yake binafsi," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >